**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Nne – Tarehe 2 Novemba, 2007**

*(Mkutano ullianza Saa 3.00 Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 44

**Baraza la Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI**

**MHE. MARGARET A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Baraza la wanaoishi na virusi vya UKIMWI au lilifufuliwa upya chini ya usimamizi wa *TACAIDS* hivi karibuni (Aprili, 2007).

(a) Je, Baraza hilo limeweza kueneza shughuli zake katika Mikoa mingapi mpaka sasa?

(b) Je, ni nini shughuli za Baraza hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu**:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, uundwaji wa Baraza la Waishio na Virusi vya UKIMWI Tanzania *(The National Council for People Living with HIV and AIDS-NACOPHA)* ulikamilishwa tarehe 18 Mei, 2007.

Shughuli hiyo ilifanyika Morogoro Mjini kwa usimamizi wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI akiwepo Kamishna wa Tume Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o, Mbunge, muuliza swali hili Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mbunge na Mheshimiwa

Kidawa Hamid Saleh, Mbunge. Mkutano huo wa siku tatu (3) uliwahusisha wawakilishi wa waishio na virusi vya UKIMWI kutoka mikoa yote 21 ya Tanzania Bara. Baraza linaongozwa na Bodi yenye wanachama wanaowakilisha Mabaraza ya Wilaya.

Hata hivyo mpaka hivi sasa kwa taarifa zilizopo Wilaya zilizounda Mabaraza hayo ni Singida Mjini na Singida Vijijini tu. Maandalizi ya kufikia azma hiyo katika Wilaya nyingine zilizobaki yanaendelea vizuri. Shirika la Umoja wa Mataifa na Wahisani wengine wanaosaidia kwenye mwitikio wa mapambano dhidi ya UKIMWI, wamelipatia Baraza hilo wataalam wawili kusaidia nao kazi. Aidha Baraza linapata msaada wa utaalam na fedha kutoka mpango wa kudhibiti UKIMWI katika Maziwa Makuu *(Great Lakes Initiative on HIV and AIDS – (GLIA*).

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za Baraza la Waishio na Virusi vya UKIMWI Tanzania (*NACOPHA)* ni kufanya uraghbishi, kutoa taarifa na elimu sahihi juu ya haki na wajibu wa waishio na virusi vya UKIMWI kwa kukuza uwezo wa wanachama wake na kuratibu shughuli zao ili waweze kushiriki kwa umakini katika mwitikio wa Taifa dhidi ya UKIMWI. Baraza linatambua na kutoa mchango wake katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kwenye maeneo ya kuzuia maambukizi mapya tiba na huduma mbalimbali kwa lengo la kupunguza athari za UKIMWI.

Shughuli nyingine za Baraza hilo ni kuimarisha mahusiano yake na Serikali hususan Serikali za Mitaa, Asasi zisizo za Kiserikali, Mashirika ya Kimataifa kama vile Mfuko wa kupambana na Kifua Kikuu, Malaria na UKIMWI *(Global Fund),* Mpango wa kudhibiti UKIMWI katika Maziwa Makuu *(GLIA), Clinton Foundation* na pia mabaraza ya nchi nyingine za Afrika Mashariki na kwingineko Duniani.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pongezi kubwa kwa mpango mkubwa wa kuanzisha Mabaraza yatakayosimamia masuala ya wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Nikumbushe tu kwamba kwa kuwa pamekuwa na kampeni ya kuhamasisha wananchi kupima virusi vya UKIMWI iliyoanzishwa na Mheshimiwa Rais mwenyewe na Wilaya ya Kongwa katika Mkoa wa Dodoma tukawekeana malengo ya kupima wananchi 30,000.

Katika hao asilimia 84 wamekwishapima katika Wilaya ya Kongwa ambayo ni mafanikio makubwa sana. Lakini kwa wale ambao wamepatikana na matatizo haya hakuna mashine ya *CD4* ambayo ipo katika Wilaya ya Kongwa, wakati Wilaya nyingine zote za Mkoa wa Dodoma zinazo mashine ya aina hii. Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri katika zoezi hili si tu kwa Wilaya ya Kongwa lakini zile Wilaya nyingine ambazo hazina mashine hii.

Je Serikali ina mpango gani wa kusaidia kupatikana kwa kifaa hicho muhimu ili wale waliojitokeza waweze kupata huduma inayotakiwa?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa majibu ya nyongeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri labda ungeweka vizuri kipaaza sauti kusudi usikike. Inaonekana sauti yako haisikiki vizuri. Labda mngemsaidia hapo, Mheshimiwa Karamagi labda mngemsaidia kwenye hivyo vipaza sauti vingine.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe majibu ya nyongeza ya swali lililoulizwa na Mheshimiwa Ndugai na napenda nimpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa majibu mazuri aliyotoa. Oh! Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kipimo cha *CD4* ni muhimu katika kutambua wagonjwa gani tuanze kuwatibu na niseme tu kwamba ni kipimo chenye gharama zaidi ya shilingi milioni 77 na tunajaribu kupata hivi vipimo katika maeneo yote ambayo hii huduma inatolewa. Hadi sasa tumeweza kufikia kila Mkoa. Kila Mkoa unacho hiki kipimo na Wilaya 30 zimeshapata. Kwa hiyo, jinsi uwezo wa Serikali utakavyopatikana nia ni nzuri kabisa kwamba Wilaya na hatimaye kila Kata, kila Kituo cha Afya kiweze kupata hii mashine.

Na. 45

**Mali zilizomilikiwa na Chama na Serikali kabla ya Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa kabla ya kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, hapakuwa na mgawanyo wa shughuli za Chama na Serikali, na kwa kuwa Watanzania kwa ujumla walikuwa wamefanya vitu vingi kwa pamoja kama vile kujenga majengo ya Ofisi yaliyotumiwa na Kiongozi/Viongozi wa Chama na Serikali kwa kila ngazi ya utawala; walimiliki mashamba na viwanja, viwanja vya michezo na mali nyingine mbalimbali na kwa kuwa kabla ya kuingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa Tume ya Nyalali pamoja na mambo mengine ilipendekeza kuwa mali hizo zilizotengenezwa na Watanzania kwa umoja wao zikabidhiwe Serikali:-

(a) Je, ni mali zipi kwa eneo na jina zilirejeshwa Serikalini ili zimilikiwe na Watanzania wote bila kujali itikadi za vyama vyao?

(b) Je, katika Wilaya ya Karatu, ni mali zipi zilikabidhiwa Serikalini?

(c) Je, Serikali iko tayari kufanya tathmini upya ili kujua ni mali zipi kwa mwaka 1992 zilikuwa za Watanzania wote ili kuona kama mgawanyo wa haki kati ya Chama Tawala na Serikali ulifanyika na kama haukufanyika, markebisho yapasayo yaweze kufanyika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Watanzania kwa ujumla wao wamekuwa wakifanya shughuli nyingi kwa pamoja. Wakati wa kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi mali za Serikali zilibaki Serikalini na zile za CCM zilibaki CCM. Baadhi ya mali ambazo zilichangiwa na wananchi na wana CCM ambazo zimebaki kuwa mali za CCM na CCM ina hatimiliki zake ni pamoja na viwanja vya mpira kwa mfano:-

1. Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine, Mbeya;
2. Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza;
3. Uwanja wa Jamhuri, Dodoma;
4. Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha; na
5. Uwanja wa Mkwakwani Tanga. *(Makofi)*

Pamoja na hayo viwanja hivyo, samahani. Pamoja na hayo, viwanja hivyo vinatumiwa na wananchi wote bila kujali itikadi zao kichama. Pia kati ya mali ambazo zilichangiwa na wana CCM na wananchi wengine kwa ujumla ni jengo la Chimmwaga ambalo CCM imelikabidhi kwa Serikali kwa ajili ya kufungua Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 Wilaya ya Karatu ilikuwa ni moja tu Tarafa ndani ya Wilaya kubwa ya Mbulu ambayo baadaye iligawanyika katika Wilaya nne, na kwa taarifa tulizonazo haikuwa na *register* ama orodha ya kumbukumbu ya mali zilizohakikiwa ili kuwawezesha kutambua mali zipi zilikuwa za Serikai na zipi zilikuwa ni za Chama cha Mapinduzi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni haja ya kufanya tathmini upya kwani katika vikao vilivyotangulia katika Bunge hili maelezo bayana yalikwisha tolewa kuhusu jimbo hili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Kwanza ieleweke kwamba yaliyotolewa na Tume ya Jaji Nyalali, yalikuwa ni mapendekezo. Nasisitiza, mapendekezo. Sasa kuhusu suala la msingi sehemu (b) ni kwamba wakati tukiingia katika vyama vingi hakukuweko na Wilaya ya Karatu na katika Wilaya ya Mbulu kwa ujumla wake wakati huo, hakukuwa na mali yoyote ambayo ingeweza ikagawiwa Serikalini. *(Makofi)*

Ninachokumbuka ni kwamba baadaye Wilaya ya Karatu ilipoundwa Chama Wilaya ya Mbulu mali ambayo iliona igawie kwa Chama Wilaya ya Karatu ilikuwa viti 150 tu vya ukumbi wa mkutano.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Duniani kote mgawanyo wa mali ni msingi wa mgogoro. Je, Mheshimiwa Waziri ataeleza Bunge hili ni chombo gani kilifanya uhakiki kufuatana na mapendekezo ya Jaji Nyalali kutathmini kati ya mali hizo zilizokuwa zimetengenezwa na wananchi wote na akapendekeza za Serikali zile za wananchi wote ziende Serikalini na zile za CCM zirudi Serikalini, chombo gani kiliahikiki baada ya mfumo wa vyama vingi kuona hizi ni za CCM, hizi ni za Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Mheshimiwa Waziri ana taarifa kwamba wiki ya tatu ya mwezi Julai 1992 baada ya Sheria ya kupitishwa ya mfumo wa vyama vingi kutoka Makao Makuu ya CCM Dodoma zilitumwa Tume nchi nzima na wakaandikisha mali zote zilizokuwepo bila kuwashirikisha wananchi, wala kumhoji yoyote kwamba ni ipi ya CCM ipi ya wananchi. Waziri atatupa taarifa kwamba taarifa hiyo inapatikana lini na kama yuko tayari kuitoa Bungeni? Je, swali linarudia. Je, Waziri yuko tayari kutoa taarifa hiyo sasa Bungeni kujua kama taarifa ya Tume ile ilifanya haki au siyo haki? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, juu ya Mhakiki Mali ni wazi Serikali ina Mhakiki Mali wake ambaye huyo ndiyo anapaswa kuhakiki mali zote za Serikali. *(Makofi)*

Pili, Taarifa kwamba wiki ya tatu ya mwezi Julai, mwaka 1992 Chama cha Mapinduzi kilituma Wajumbe nchi nzima kufanya ukaguzi wa kuhakiki mali zake na zile za Serikali kwa kweli kwa sasa hivi siwezi kukiri kwamba ninazo au sina. Ilipaswa liwe nalo ni swali pekee ambalo lingepaswa kutafutiwa utafiti wa kina. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ambaye sasa anakaimu nafasi ya Waziri Mkuu kama Kiongozi wa Serikali Bungeni. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwanza swali lake la kwanza la Bwana Slaa ni kwamba Serikali ndiyo iliyogawa mali hiyo ya Chama na Serikali.

La pili, Tume iliyotumwa kutembelea nchi nzima ilikuwa ya Chama cha Mapinduzi kuhakiki mali zake. Lakini nasema kwamba wakati wa kuchangia mali hizi waliochangia mali hizi walichangia kwa hiari yao wenyewe, hawakulazimishwa na wale walioondoka, wameondoka kwa hiari yao wenyewe. Na kwa hivyo nafikiri si vema sasa hivi kukumbusha kilio matangani. Wananchi wameridhika nayo na tuendelee na kujenga umoja wetu kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Mnyaa hukusimama wakati tunaanza swali hili. Kwa hiyo, kama hili swali linahitaji mjadala wa ziada liletwe kwa taratibu zinazotakiwa.

Na. 46

**Club za kupambana na Rushwa**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO (K.n.y. MHE. DR. ZAINAB A. GAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kupambana na rushwa limepewa kipaumbele kikubwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa hivi sasa baadhi ya Shule za Sekondari zimeanzisha *Club* za wanafunzi za kupambana na rushwa pamoja na masuala ya UKIMWI:-

(a) Je, mpaka sasa kuna shule ngapi zilizoanzisha *Club* hizo?

(b) Je, Serikali inaona kuwa mpango huu ni mzuri, kama ndiyo, kwa nini isianzishe somo la Utawala Bora na Uwajibikaji pamoja na UKIMWI mashuleni, pamoja na uanzishaji wa vilabu hivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naomba nimjibu Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mbunge wa Kibaha lenye sehemu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:- Lakini kabla ya hapo naomba nitoe ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, athari za rushwa zinamgusa kila mwanajamii bila ya kujali umri, rika au jinsia yake. Rushwa ni kikwazo cha harakati za kuleta Maendeleo kwa

Watanzania. Serikali nayo imechukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na tatizo hili. Makundi yote ya kijamii yanapaswa kushiriki kikamilifu katika kuzuia na kupambana na rushwa. Taasisi yetu ya Kuzuia na Kupambana na rushwa (TAKUKURU) ambayo ndiyo yenye jukumu la kuongoza mapambano dhidi ya rushwa nchini, hutumia mbinu mbalimbali kuelimisha na kuwashirikisha wanajamii wa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanafunzi walioko shuleni katika kuzuia na kupambana na rushwa.

Njia mojawapo inayotumiwa na TAKUKURU ni kuwashirikisha wanafunzi katika mapambao dhidi ya rushwa na kuanzisha klabu za Wapinga Rushwa katika Shule za Sekondari katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Mpango huu ulizinduliwa rasmi na TAKUKURU tarehe 11 Mei, 2007 ambapo TAKUKURU hushirikiana na klabu hizo katika kutoa elimu na ushauri. Klabu za aina hii zimebainika kuwa na uwezo wa kuwajenga wanafunzi kimaadili, hivyo kuwawezesha kutambua nafasi na wajibu wao katika mapambano dhidi ya rushwa na madhara ya rushwa yenyewe kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa shule za sekondari 1,219 katika mikoa yote Tanzania Bara zimeanzisha klabu za wanafunzi za kupambana na rushwa. Uanzishwaji wa klabu za aina hii kwa shule zilizobaki unaendelea.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzishwa kwa somo la Utawala Bora na UKIMWI mashuleni, napenda kusema kwamba masuala mtambuka *(cross cutting issues)* kama vile Rushwa, UKIMWI, Utawala Bora na Uwajibikaji yanafundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu kupitia mitaala mbalimbali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambayo huandaa kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania. Kwa mfano, masuala kuhusu rushwa, maadili na Utawala Bora yanafundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu kama ifuatavyo:-

(i) Katika Elimu ya Msingi, Utawala Bora unafundishwa katika darasa la Nne, Tano na Sita, kwenye somo la uraia ambapo kuna mada mahsusi ya Utawala Bora.

(ii) Katika Elimu ya Sekondari, hususan kidato cha kwanza hadi cha Kidato Nne kwenye somo la *Civics,* ipo mada ya *Prevention of Abuse of Power in Public Service* ambayo hufundishwa katika kidato cha Pili na cha tatu.

(iii) Katika Elimu ya Sekondari, kidato cha Tano na Kidato cha Sita suala la rushwa linafundishwa kama *Socio Economic Problem* chini ya mada ya *Socio-Economic Issues* kwenye somo la *General Studies.*

(iv) Katika vyuo vya Ualimu ngazi ya Cheti kuna mada za Maadili na Matumizi mabaya ya Madaraka ambazo zinafundishwa kwenye somo la Uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wanafunzi kufundishwa masuala haya shuleni, tunawasihi sana wazazi na jamii nzima kukumbuka wajibu wa kuwalea vyema watoto na vijana wao na kuwafundisha maadili meema, kwani uadilifu wa mtu unajengwa tangu akiwa mdogo.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina mikakati mikubwa sana ya kupambana na rushwa pamoja na kuhakikisha Utawala Bora unazingatiwa katika maeneo yetu. Je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuunda Kamati mbalimbali za kushughulikia rushwa na Utawala Bora katika ngazi za Vijiji na Kata ili wananchi waridhike na Serikali yao katika kupambana na suala hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimrejeshe Mheshimiwa Maneno na Waheshimiwa Wabunge kwenye Sheria yetu mpya inayounda Taasisi ya Kupamba na Kuzuia Rushwa ya mwaka huu ambayo ilianza rasmi tarehe 1 mwezi wa saba mwaka huu.

Pamoja na mkakati wa kupambana na rushwa nchini wa mwaka 2006 hadi 2011. Sheria hii na mkakati niliyoutaja unahusisha kila mwananchi, kila mwananchi anataka amiliki mapambano dhidi ya rushwa. Na ndiyo maana mkakati wa kupambana na rushwa wa 2006 mpaka 2011 unatarajia kuanzisha Kamati za Maadili katika Idara za Serikali, katika Halmashauri za Wilaya na tunaelekea kwenye ngazi ya Vijiji, ngazi ya Kata, ngazi ya Tarafa. Hata hivyo kama nilivyosema maadili na uadilifu kwa ujumla wake unaanzia katika familia moja moja.

Na. 47

**Madhara ya Uharibifu wa Mazingira**

**MHE. PARMUKH S. HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanywa na nchi zinazoendelea katika mambo ya viwanda duniani inakabiliwa lna joto lisilo la kawaida ambalo sote tunalishuhudia:-

(a) Je, kwa nini nchi ya Marekani hailazimishwi kusaini mkataba wa Kyoto?

(b) Je, joto hilo likiachwa kuendelea, nchi na bahari yetu inaweza kuathirika vipi hapo baadaye?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA (PROF. MARK J. MWANDOSYA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh S. Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, napenda kutoa maelezo utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili linafanana, kimaudhui, na swali Na. 15 lililoulizwa na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, lililojibiwa juzi tarehe 31 Oktoba 2007. Ni kweli kwamba shughuli za viwanda na uchukuzi hasa katika nchi tajiri zinachangia kwa kiasi kikubwa tatizo la ongezeko la joto duniani *(global warming).* Hali hii inachangiwa na gesijoto *(greenhouse gases)* ambazo husababisha ongezeko la joto la dunia na mabadiliko ya tabianchi. Gesijoto hizi ni pamoja na hewa mkaa *(Carbon-dioxide) Methane,* na *Nitrous Oxide* na nyingine ni *Sulphur Hexafluorid, Hydrofluorocarbons* na *Perfluorocarbons.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Kimataifa imeanzisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na itifaki ya Kyoto ya mkataba huu ili kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa kujibu sehemu (a) na (b) ya swali kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani imesaini Mkataba wa mabadiliko ya Tabianchi lakini mpaka sasa imekataa kuridhia Itifaki ya Kyoto. Sababu kubwa ya kutoridhia Itifaki ni kwamba uchumi wa Marekani unategemea sana matumizi ya mafuta. Kuna dhana kwamba kwa baadhi ya sekta zenye ushawishi mkubwa Marekani kwamba kuridhia itifaki hii kutahatarisha uchumi wake.

Hata hivyo Sweden imeonyesha kwamba nchi inaweza ikapunguza utoaji gesijoto na uchumi wake ukakua. Kwa mfano kati ya mwaka 1990 na mwaka 2005, Sweden ilipunguza utoaji gesijoto kwa asilimia 7, na uchumi wake ulikua kwa asilimia 36.

Kuridhia au kutoridhia mkataba wa kimataifa ni hiari ya nchi husika. Mikataba hii hailazimishi nchi yeyote kuiridhia. Hata hivyo kuchukua uamuzi wa Marekani kutoridhia itifaki ya Kyoto kunakwamisha jitihada za Jumuiya ya Kimataifa katika kupambana na tatizo la ongezeko la joto la dunia na madhara yake. Kwani Marekani huzalisha takriban asilimia 23 ya gesijoto zote duniani. Jitihada mbalimbali zinafanywa na Jumuiya ya Kimataifa kuishawishi Marekani kutoa mchango wake katika kupunguza ongezeko la joto la dunia kwa kuridhia Itifaki ya Kyoto.

Dalili njema zimeanza kuonekana. Baadhi ya majimbo ya nchi hiyo kama vile California yameanza kuchukua hatua za kisheria za kupunguza uzalishaji wa gesijoto. Baraza la Kutunga Sheria la Marekani *The Congress* limeanza mjadala wa awali wa suala

hili muhimu, leo hii Mameya wa Miji mikubwa 110 nchini Marekani wanakutana Seato kuzungumzia utekelezaji wa maudhui ya Itifaki ya Kyoto na sasa na Serikali ya Marekani sasa imeanza kuzungumzia suala hili.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara ya ongezeko la joto la dunia ni makubwa hasa katika nchi maskini kama Tanzania. Madhara haya ni pamoja na:-

(i) Kuongezeka kwa matukio ya ukame yanayosababisha kupungua sana kwa nishati ya umeme na upungufu wa chakula;

(ii) Kuongeza kwa mafuriko;

(iii) Mabadiliko ya majira ya mwaka;

(iv) Kupungua kwa kina cha maji katika maziwa;

(v) Kuongezeka kwa kina cha bahari kunakosababisha; kulika kwa fukwe, kupotea kwa visiwa vidigo na baadhi ya visima maeneo ya pwani kuingiliwa na maji ya chumvi; na

(vi) Kuongezeka kwa maambukizi ya magonjwa kama malaria katika maeneo ya milimani ambako zamani ugonjwa huu haukuwa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni baadhi tu ya madhara yanayoikumba nchi yetu yanayotokana na ongezeko la joto la dunia ambayo tayari yana athiri jitihada za Serikali za kuleta maendeleo ya kuondoa umasikini kwa wananchi wake. Mabadiliko ya tabia ya nchi yameelezwa kuwa ni changamoto kubwa inayokabili dunia karne hii. Kimaendeleo, kiusalama, kisiasa na kimazingira. Namshukuru Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kuuliza swali hili la msingi *(Makofi).*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya kina ya kuridhisha na kitaalamu ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa Kuwa, gesijoto hizi zinavyochangia kwenye uharibifu wa mazingira zinatokana vile vile na mioto kichaa na mioto ambayo inachomwa kwa ajili ya kuandaa mashamba katika nchi zinazoendelea pamoja na Tanzania. Je, ni mikakati gani ambayo Wizara inaweka au imeweka kudhibiti mioto kichaa ambayo iko kila mahali katika nchi hii na inachangia kwa kiasi kikubwa kwenye *green house gases?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA (PROF. MARK J. MWANDOSYA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa na mwana mazingira kama ifuatavyo:-

Ni kweli tunayoita mioto vichaa, huongeza kwa kiwango kikubwa gesi joto inayokwenda hewani, lakini vile vile huleta madhara makubwa si kwa mazingira tu lakini vile vile kwa mali na maisha ya binadamu na viumbe wengine. Itakumbukwa Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba moja ya changamoto kubwa zilizomo katika mkakati wa Serikali wa hifadhi ya ardhi na vyanzo vya maji ni kuzuiya mioto vichaa. Na hili ni jambo ambalo maelekezo yametolewa kwa Halmashauri na vile vile kwa Wakuu wa Wilaya kuhimiza uelewa mkubwa wa jamii kuhusu suala hili ambalo ni tatizo kubwa.

Na tatizo hili si Tanzania tu, hata Marekani limetokea katika wiki iliyopita, ni tatizo kubwa kweli kweli. Lakini wao wanaweza kumudu hili suala lakini sisi hatuwezi kumudu. Kwa hiyo, tutaendelea kuelimisha lakini wakati huohuo kuchukua hatua za kisheria kwa wale wanaopatikana na hatia ya kuchoma mioto vichaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengine ya nchi niliyopitia ati ukichoma moto, moto huo ukienda mbali basi utaishi maisha marefu zaidi kuliko moto unaoishia karibu. Lakini hizi ni kwa kweli hisia potofu sana ambazo elimu ndio jawabu lake. *(Makofi)*

Na. 48

**Uharibifu wa Mazingira ya Mto Ruhuhu**

**MHE. CAPT. JOHN KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mto Ruhuhu ni mazalia muhimu kwa samaki katika Ziwa Nyasa na kwa kuwa katika vyanzo vya mto huo wapo wachimbaji wadogo wadogo wa vito wanaofanya shughuli za uchimbajhi na hivyo kuchuja udongo kwa kutumia zebaki kwenye vyanzo vya mto huo, hali inayoleta uharibifu mkubwa wa mazingira:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia hali hiyo isiendelee ili kunusuru samaki na binadamu wanaoyatumia maji ya mto huo kwa maisha yao ya kila siku?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kazi wanazofanya wachimbaji wadogo wadogo kwa kuchuja udongo katika vyanzo vya mto huo ndiyo mwanzo wa kuangamiza kabisa mto huo?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA (PROF. MARK J. MWANDOSYA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama yafuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bonde la Mto Ruhuhu, dhahabu huchomwa katika eneo la Lukarasi, Kata ya Kihangi Mahuka, Tarafa ya Mbinga Mjini. Eneo linalozunguka Mto Ruhuhu au bonde la mto Ruhuhu pia lina madini ya vito aina ya *Sapphire* ambayo kwa sasa yanachimbwa na wachimbaji wadogo.

Shughuli za uchimbaji na uchujaji wa madini ya vito hufanyika kwa kutumia maji. Baadhi ya wachimbaji husafisha udongo huo moja kwa moja mtoni kwa ajili hiyo husababisha udongo mwingi kubaki mtoni, hali ambayo husababisha baadhi ya mito kujaa zebaki yaani *sediments* na kushindwa kutiririsha maji yake kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo mikakati mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira katika maeneo ya mito na vyanzo vya maji, mto Ruhuhu ukiwa mmojawapo. Mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji uliopitishwa na Serikali Machi mwaka 2006 unatoa msisitizo wa pekee kuhusu kuzuia uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za uchimbaji wa madini. Wakuu wa Wilaya na Halmashauri za Wilaya na Miji wameelekezwa kusimamia utekelezaji wa Mkakati kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Usalama wa Raia, na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kuhusu eneo aliloulizia Mheshimiwa Capt. Komba Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati na Madini imekuwa ikitoa elimu ya mazingira na uchimbaji unaozingatia sheria na kanuni. Wachimbaji wadogo wa madini ya vito wanapaswa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya uchenjuaji wa madini hayo ili kuepuka uharibifu wa mito kwa kuingiza zebaki na udongo katika mito hiyo. Wizara ya Nishati na Madini vile vile hufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu sheria na kanuni za uchimbaji madini na hifadhi ya mazingira. Ofisi ya Madini iliyopo Songea imeendelea kuhakikisha kwamba shughuli za uchimbaji wa madini katika vyanzo vya Mto Ruhuhu zinazingatia hifadhi ya mazingira. Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga inashauriwa kutunga sheria ndogo ili kuweka msingi wa uchimbaji mdogo ulio endelevu na usioathiri mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya madini kwa kushirikiana na Baraza la uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, *NEMK* na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* na wadau wengine, wanaandaa rasimu ya namna bora ya kudhibiti matumizi ya zebaki hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu amechaguliwa kuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi, Mheshimiwa Capt. John Komba, amekuwa mtetezi mkubwa wa Maendeleo ya Bonde la Ziwa Nyasa katika maeneo mbalimbali kama vile utalii, uvuvi, uchukuzi na mazingira. Tunamshukuru sana.

**MHE. CAPT. JOHN KOMBA:** Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa vile uharibifu umekuwa ni mkubwa sna katika bonde hilo, na kwa vile Mheshimiwa Waziri amesema mikakati inafanywa ili hali iwe nzuri. Hii mikakati itaanza lini hasa?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA (PROF. MARK J. MWANDOSYA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Capt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi kama ifuatavyo:-

Naomba kuthibitisha kwamba utekelezaji wa mkakati wa Serikali unaohusu hifadhi ya ardhi na vyanzo vya maji umeanza kutekelezwa. Hivi karibuni katika ripoti nilizonazo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini alikuwa maeneo ya Ruvuma basi huenda hakupitia maeneo hayo lakini hii ilikuwa ni moja katika utekelezaji wa mkakati huo katika sekta ya madini.

Lakini naamini kabisa kama hajaenda huko basi mimi mwenyewe au Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini tutakuja huko kusimamia utekelezaji wa Mkakati huo. Asante.

Na. 49

**Ugonjwa wa Fistula**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya akina mama wakati wa kujifungua hupata matatizo ya uzazi na kuwasababishia ugonjwa wa fistula yaani hali ya kutokwa na haja ndogo na kubwa bila kujitambua.

(a) Je, ni nini chanzo cha maradhi hayo?

(b) Je, ni nini tiba yake ?

(c) Je, ni haspitali ngapi zinafanya upasuaji wa ugonjwa huo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Fistula ni tundu linalotokea katika misuli kati ya uke na kibofu cha mkojo au kati ya uke na njia ya haja kubwa au sehemu zote mbili baada ya kujifungua. Chanzo cha tatizo hili ni mgandamizo wa kichwa cha mtoto kwa muda mrefu katika njia ya uzazi.

Mgandamizo huo huzuia mtiririko wa damu kuingia katika misuli hali ambayo husababisha misuli hiyo kufa na hatimaye tundu hutokea. Sababu zinazosababisha

mgandamizo wa kichwa cha mtoto katika njia ya uzazi ni pamoja na uzazi pingamizi unaosababishwa na mtoto kukaa vibaya tumboni, mtoto kuwa mkubwa  na mzazi kuwa na nyonga ndogo. Tatizo hili la nyonga ndogo hujitokeza zaidi kwa Wanawake wenye umri mdogo chini ya miaka 20 au wanawake wafupi wenye urefu chini ya sentimeta 150. *(Makofi)*

(b)  Mheshimiwa Mwenyekiti, fistula hutibiwa kwa njia ya upasuaji.

(c) Kuna hospitali 21 zinazotoa huduma ya upasuaji kwa Wanawake wenye matatizo ya fistula. Kati ya hizi, hospitali 14 hutoa huduma wakati wote ambapo hospitali 7 hutoa huduma hiyo kwa vipindi maalum. Orodha ya hospitali zinazotoa huduma hii ni kama ifuatavyo:-

**MHE. MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa orodha ni ndefu kidogo, mimi nafikiri ungetusaidia Wabunge wote tukaipata kwa maandishi itatupa nafasi ya kujifunza zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Sawa Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya hospitali 14 ambazo hutoa huduma za fistula zitatolewa kwa Wabunge wote kwa maandishi na orodha ya hospitali ambazo hutoa huduma hiyo kwa vipindi maalum  pia nitawapatia  baadaye,  ahsante sana.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, kuna baadhi ya wanaume ambao wake zao wamepata ugonjwa huu kutokana na matatizo ya kujifungua. Wanaume wao huwatenga na hata kudiriki kuwaacha badala ya kuwasaidia, jambo ambalo linawadhalilisha sana wanawake. Je, Serikali  ina kemea vipi wanaume wa aina hiyo?

Swali la pili, kwa kuwa, kuna baadhi ya watu wanahusisha maradhi haya na imani za ushirikina na kuacha kwenda hospitalini, badala yake huenda kwa waganga wa kienyeji. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza kuelimisha juu ya maradhi haya hasa huko vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii,  naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Faida kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, ni kweli kwamba kuna baadhi ya waume huwaacha wake zao na kuwatelekeza mara wapatapo na tatizo hili la fistula. Napenda niseme niwaambie Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu  na wananchi popote wanaposikiliza kwamba kama nilivyojibu katika jibu langu la awali ni kwamba ugonjwa wa fistula unatibika. Kwa maana hiyo ningependa kutoa ushauri kwamba, mara mwanamme au mume atakapoona mke wake kapata tatizo hili mara moja ampeleke hospitali, kwasababu atakapofanyiwa operesheni yule mama atapona vizuri na

ataweza kushiriki tena zaidi, ataweza kushiriki kwa ukamilifu katika tendo la ndoa hivyo hakutakuwa na sababu ya kumzuilia asiweze kukaa na mke wake *(Makofi).*

Swali la pili Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, ni kweli kuna baadhi wanahusisha na masuala haya na ushirikina, lakini nitakachotoa kama angalizo na wito kwa wananchi ni kwamba, wakina mama watakapokuwa wajawazito nawashauri waende hospitali wakifika hospitalini watapimwa na kuonekana urefu wao kama unatosheleza na kama ni wafupi chini ya sentimita 150 huwa watafanyiwa uchunguzi.

Lakini kwa mimba ya kwanza kawaida wakina mama wanapimwa nyonga zao na kufahamishwa kama nyonga zile zinatosheleza au hazitoshelezi kwa kuzaa. Hivyo watapewa ushauri waweze kujifungua kwa njia gani na watajiandaa kikamilifu kulingana na hali yao. Wale wenye nyonga ndogo wakazae kwa operesheni au kwa msaada wa wataalamu wa hospitali. *(Makofi).*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mwenyezi Mungu alipowaumba binadamu alimchagua mwanamke kwamba kupitia yeye na maungo yake ndipo binadamu wote waumbwe. Na kwa kuwa, kwa hali hiyo kuna *side effects* nyingi sana za maungo ya mwanamke kutumika kutengeneza binadamu na kumleta duniani kwa hali ngumu na uchungu na hatari kubwa. Je, serikali hasa kupitia Wizara ya Afya, kwa kuwa inaelewa kwamba kuna *side effects* nyingi za maungo ya mwanamke kumwumba binadamu na kumleta duniani, ina mikakati gani ya kutayarisha dawa za kuwasaidia wanawake vijijini na mijini ilikujikinga na maradhi mengi yanayotokana na *side effects* za kuumba binadamu kupitia kwenye matumbo yao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maungo ya mwanammke kama alivyodai Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ni kweli yameumbwa kuweza kutengeneza mtoto. Na kwa kujifungua ni lazima mwanamke atajifungua kwa uchungu kwa sababu ndivyo ilivyokuwa *process* ya kuzaa ni lazima uchungu uwepo na ndio maana mtoto atoke. Sijui kama Mheshimiwa Mbunge, aliouliza jina anaulizia vipi, lakini dawa ya kujikinga na asipate maumivu sijui kama analijua hilo. Hiyo dawa kama anataka anaweza akapatiwa lakini kwa Tanzania sisi kawaida mara nyingi hatutumii. Lakini kama ni dawa ya kujikinga na maradhi ili aweze kuzaa kiumbe mzuri huu ni ushauri ambao tuliokuwa tukiutoa kama sisi Wizara, watoto, wakina mama wanapokwenda katika hospitali wanapewa ushauri ili waweze kupunguza yale maambukizi yatakayosababisha kwamba azae mtoto mzuri. *(Makofi)*

Lakini kuzuia mama asipate matatizo ya maumivu kwakweli hilo itakuwa hakuna dawa ni lazima apate maumivu na uchungu mzuri ndio utamsababisha aweze kuzaa haraka na mtoto aweze kutoka na aweze kulia na aweze kuwa na afya nzuri *(Makofi)*.

Na. 50

**Utupaji wa Watoto**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza**:-**

Kwa kuwa idadi ya Wanawake wanao tupa watoto wao inasemekana kuwa inaongezeka:-

(a) Je, ni watoto wangapi wa kiume na wa kike waliookotwakutoka sehemu mbalimbali kuanzia mwaka 2005 – 2007?

(b) Je, ni watoto wangapi kati ya hao waliookotwa wakiwa hai na ni wangapi walikuwa wamekufa?

(c) Je, ni Mikoa ipi iliyoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto waliotupwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa idadi ya watoto wanaotupwa inazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na sababu mbalimbali za kijamii. Kwa mujibu wa taarifa ya kesi zilizoripotiwa katika Wizara yangu, katika kipindi cha mwaka 2005 – 2007 jumla ya watoto 192 waliokotwa wakiwa hai na kuhifadhiwa katika makao mbalimbali kwa ajili ya ulinzi, malezi na matunzo. Kati ya watoto hao wavulana walikuwa ni 102 na wasichana 90. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye kipengele (a) hapo juu, jumla ya watoto waliookotwa wakiwa hai katika kipindi hicho ni 192. Wizara yngu haina taarifa za watoto waliookotwa wakiwa wamekufa. Hii ni kwasababu suala la watoto wanaotupwa hushughulikiwa na Wizara ya Usalama wa Raia kwa kushirikiana na Wizara yangu. Watoto wanaookotwa wakiwa hai huletwa Wizarani kwangu kwa taratibu na matunzo na wale wanaookotwa wakiwa wamekufa hushughulikiwa moja kwa moja na Wizara ya Usalama wa Raia.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa inayoongoza kwa utupaji wa watoto ni Dar-Es-Salaam, ikiwa na jumla ya watoto 139, ukifuatiwa na mkoa wa Mwanza watoto 18 na Kagera watoto 11.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, kina mama hawa wanaotupa watoto, sababu mojawapo inayowasababishia ni akina baba kutokuwa tayari kutoa huduma baada ya kuwaona wameshapata ujauzito.

(a) Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kina baba hawa wakibainika na wao kuchukuliwa hatua?

(b) Je, watoto wanao okotwa wakiwa hai, endapo mama amebainika akachukuliwa hatua, labda kupewa adhabu ya kifungo. Je, anapomaliza adhabu ya kifungo anaruhusiwa kwenda kuchukua mtoto wake akaendelea kumtunza?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Kasembe kama ifuatavyo.

Swali la kwanza, ni kweli kwamba baadhi ya sababu zinazosababisha wakina mama kutupa watoto ni kwamba wale wanaume wanakataa kutoa msaada wakati wanapotambua kwamba wamewapa ujauzito. Ninachoweza kusema Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwamba, akina baba wanaowapa wakina mama ujauzito wanatakiwa na wanapaswa kukubali zile mimba ili waweze kuwatunza.

Lakini vile vile Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa wito kwamba kuzaa mtoto na kupata ujauzito ni kitu ambacho kinaweza kuzuilika. Kama unakuwa huna uhakika na yule mwenza wako kwamba ukipata ujauzito atakusaidia ni vizuri kufuata njia ya uzazi wa mpango na kutumia kinga ili usiweze kupata mimba na hatimaye kusaidia usije ukapata tatizo la kukataliwa na kuweza, hatimaye kukupelekea kutupa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu ambayo anapewa mama anayetupa mtoto mara akifahamika na kama mtoto yupo hai anapokuwa anatumikia kifungo basi mtoto wake baada ya kuchunguzwa na kuonekana kwamba akili yake iko timamu, anapewa mtoto wake ataendelea kuwa na kifungo chake na wakati huohuo kuendelea kumtunza mtoto kwa sababu anatakiwa aendelee kutumikia kifungo kama ni adhabu lakini wakati huo huo amnyonyeshe mtoto wake ili aweze kukua na kuishi.

**MHE, MWENYEKITI:** Eeh, kwa kuwa suala la uzazi ni suala la akina baba na akina mama naomba nitoe nafasi sasa kwa Mbunge wa jinsia ya kiume, Mheshimiwa Kimaro tafadhali.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swali lifuatalo. Hawa watoto ni sawa na watoto wa mitaani. Na mara nyingi hulelewa kwenye vituo maalum, sasa swali. Baada ya kutimiza miaka 18 ama kuwa watu wazima, hawa watoto ambao hawana baba, mama, wala koo zao huwa wanapelekwa wapi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kimaro, la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kama alivyosema watoto hawa si kama watoto wa mitaani kwa sababu mtaa hauna mtoto, mtoto ana baba na mama yake. Kwa hiyo naomba niseme hakuna mtoto wa mitaani mtoto ni wa kwetu sisi wote. Lakini vile vile watoto hawa wanapokuwa kwenye vituo maalumu wanapata uangalizi, lakini inapofikia mtoto ana miaka 18, mtoto huyu anakuwa ameshakuwa ni mtu mzima kwa hiyo anaweza akasaidiwa na pale anapokuwa ana Taasisi anazohudumiwa na Serikali itamhudumia. Akiweza kujitegemea basi atajitegemea kama mwananchi mwingine yeyote aliyefikisha umri wa kujitegemea.

Na. 51

**Muda wa Matumizi ya Fedha Zilizopitishwa Kwenye Bajeti ya Serikali**

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka wa fedha wa Serikali huanza mwezi wa saba na kuishia Juni kila mwaka. Na kwa kuwa, utaratibu wa kujadili na kupitisha Bajeti ya mwaka husika huchukua takribani miezi mitatu yaani kuanzia Juni katikati mpaka pale fedha za mwaka huo zinapokwenda kuidhinishwa; na kwa kuwa, kipindi hicho Serikali haiwezi kutumia fedha kwa shughuli za maendeleo mpaka bajeti iwe imeidhinishwa na Bunge hivyo miradi mingi ya Serikali huchelewa kuanza kwa takribani miezi 3 hadi 4 yaani Julai hadi Septemba kila mwaka, na kwa kuwa, kati ya Julai hadi Novemba ndio kipindi kizuri cha kutekeleza miradi mbalimbali hasa kwa ujenzi wa barabara na majengo lakini kipindi hicho hakitumiki ipasavyo Serikali hutolewa au kutumika kwa dharura kwenye mwezi Mei na Juni kila mwaka na kusababisha matumizi mabaya yasiyozingatia Sheria ya manunuzi:-

(a) Je, Serikali haioni upungufu huo wa muda na matatizo katika utekelezaji wa miradi yake kunatokana na kuchelewa kutolewa kwa fedha za Serikali hivyo miradi hushindwa kukamilika kwa muda muafaka ?

Je, Serikali inaweza kubadilisha muda wa kuwasilisha kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Serikali Bungeni ili ianze mwezi Machi na kukamilika mwezi Mei ili fedha iidhinishwe kwa wakati na kuwezesha utekelezaji wa mipango ya Serikali kuanzia mwezi Julai mwaka wa fedha unapoanza?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Saidi Nyaulawa, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Nyaulawa kwamba mwaka wa fedha wa Serikali huanza mwezi wa saba na kuishia mwezi Juni mwaka unaofuata. Ni kweli pia kwamba utaratibu wa kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali huchukua takribani miezi mitatu yaani kuanzia Juni katikati mpaka pale fedha za mwaka huo zinapoidhinishwa. Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kuchelewa kuanza utekelezaji wa miradi ya maendeleo hakutokani na sababu ya Bunge kuchelewa kuidhinisha bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba hakuna kipindi chochote ambacho miradi na kazi nyingine za serikali zinasimamishwa kwa sababu bajeti ya Serikali haijaidhinishwa na Bunge. Upo utaratibu wa kisheria unaompa mamlaka Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuidhinisha sehemu ya matumizi ya Serikali kabla bajeti haijaidhinishwa na Bunge.

Kwa mujibu wa aya ya 139 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Rais anaweza kuidhinisha theluthi moja ya bajeti itumike mpaka Sheria ya Matumizi ya mwaka huo itakapoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa, Serikali bado inatumia mpango wa *'Cash Budget'* katika kutoa fedha za matumizi wakati wa utekelezaji wa bajeti, ingawa hata chini ya mpango huu, Serikali hutoa kipaumbele kwa matumizi ya maendeleo.

Lakini ni vizuri ikafahamika pia kuwa, kuna vigezo ambavyo ni lazima vizingatiwe kabla ya fedha za maendeleo kutolewa, navyo ni kila Wizara, Idara, Mkoa na Halmashauri kuandaa na kuwasilisha taarifa zifuatazo:-

(i) Taarifa ya utekelezaji wa miradi yaani *Progress Reports* kwa kipindi kilichomalizika.

(ii) Ratiba ya utekelezaji yaani *Action Plan* kwa kipindi kijacho.

(iii) Mtiririko wa fedha yaani *Cashflow Plans.*

(iv) Hati za malipo za makandarasi kwa miradi ambayo inatekelezwa na makandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kuweka vigezo hivyo ni kuhakikisha kwamba kuna mipango mizuri na madhubuti katika kutekeleza Bajeti ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Serikali inapata thamani kwa fedha zinazotumika yaani *Value for Money*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kwamba hakuna upungufu wa muda na matatizo ya muda katika utekelezaji wa miradi ya Serikali. Hivyo, hakuna sababu ya kubadilisha muda wa kuwasilisha, kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Serikali Bungeni.

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa, Serikali ni mteja mkubwa wa bidhaaa na huduma nyingi hapa nchini. Na kwa kuwa, kutofanya matumizi na malipo kwa kipindi cha miezi 3 kama ambavyo inahitajika kwasababu malalamiko haya huwa tunapata mengi sana kutoka kwa wananchi wa kawaida na wafanyabiashara. Je, Serikali inaweza kufanya utafiti wa ndani ili kuweza kubaini hasara za kibiashara, yaani *economic impact* ambazo zinatokana na kutokufanya matumizi hayo kwa urahisi na labda hiyo taarifa iweze kuwakilishwa hapa Bungeni?

Swali la pili, kwa kuwa, kuna malalamiko mengi kutoka kwa wafanya biashara kutofanyiwa malipo katika kipindi cha Bajeti na kwa kuwa, Naibu Waziri ametueleza kwamba huwa kunakuwa na vigezo maalum ambavyo vinastahili kufuatwa ili kuweza kuidhinisha matumizi katika kipindi hicho.

Je, huwa kunakuwa na matatizo gani ndani ya Serikali kuweza kuvifikia hivyo vigezo alivyovitaja ili kuweza kuhakikisha kwamba matumizi yanafanyika kama utaratibu unavyostahili kwa mwaka mzima? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kama nilivyojibu katika swali la msingi, hakuna wakati wowote ambapo Serikali inakuwa haina pesa. Bajeti yetu ni *Cash Budget*. Kwa hiyo, mwezi wa sita kabla ya tarehe 25 pesa za miezi mitatu mpaka Septemba zinakuwa zimetolewa. Tatizo linakuwa ni Idara husika kuweza kutoa maelezo yanayoridhisha ili waweze kupewa pesa hizo.

Kwa hiyo, kama ni kweli kwamba wako wanaolalamika tunakubali kwamba tutafanya utafiti na ikidhihirika Serikali itatafuta namna ya kurekebisha tatizo hili.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh, kwa kuwa Waziri nina hakika anafahamu katika Bajeti zote za kila mwaka ambazo zifanye kazi ni Bajeti ya Maendeleo.

Hili liko katika vitabu vyote vya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kuna Wizara zingine hazipati au inapata labda asilimia 20 kwa mwaka mzima, kwa fedha ya Maendeleo. Sasa Waziri anaposimama hapa, anasema kuwa kwamba hakuna athari yoyote inayotokea sijui anataka Taifa hili tumwelewe vipi?

Na ninajua wazi kuwa kwamba…

**MHE. MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, naomba uende kwenye swali moja kwa moja

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ndio tumwelewe vipi? Na ninajua, namalizia swali, na ninajua wazi kwamba fedha zote za barabara kwa mfano ndio sasa zinafika kwenye Halmashauri. Ambapo huu ni mwezi wa Novemba.

Kwa hiyo, nataka ulieleze Bunge hili ni nini kinachofanyika? Ni nini kinachofanyika katika Wizara ya fedha ili kuhakikisha kuwa kwamba Bajeti kweli ya Maendeleo inafanya kazi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kama nilivyojibu katika swali la msingi Bajeti ya Serikali ni ya miezi kumi na mbili sio ya miezi ya tisa. Kwa hivyo kwa mwezi wa saba, nane na wa tisa pesa zinakuwa zimeshawekwa isipokuwa pale ambapo pesa hizo za wafadhili. Kwa sababu wafadhili wana vigezo maalum tatizo tunalolipata na Mheshimiwa Cheyo tukifika Dar es Salaam unaweza kuja ofisini kwangu nikakuonyesha.

Tatizo tunalolipata ni la utekelezaji kwamba zile idara ambazo zinatekeleza miradi husika huwa hawajaandaa taratibu zinazokubalika wakitegemea kwamba kwa sababu mwaka umepita basi tutapata pesa. Tunachoshauri idara zote zinazohusika wahakikishe kwamba wanawakilisha karatasi na makabrasha yanayotakiwa na wanajua nini kuwasilisha wakifanya hivyo hakuna mradi wowote ambao unaweza ukakwama. Nakubali na kwamba ni kweli kwamba iko miradi ambayo inachelewa lakini haikuchelewa kwa sababu Hazina au Serikali kwa ujumla haukupewa pesa, ni kwa sababu watekelezaji hawakutekeleza inavyotakiwa.

Na. 52

### Suala la Watanzania Wawili Waliouawa Nchini Marekani

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, palikuwepo na tuhuma za kuuawa Watanzania wawili (2) huko Marekani (Kijana wa kiume na mchumba wake) na Serikali ikaahidi kufuatia suala hilo kwa undani:-

Je, Serikali imefuatilia vipi suala hili na inawaambia nini Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. SEIF ALI IDD)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ukifuatia kwa karibu Maendeleo ya uchunguzi wa mauaji ya raia wawili wa Tanzania, Bwana Walter Mazula na Bi. Vonetha Nkya, yaliyotokea huko Detroit, Michagan, Septemba 22, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Ubalozi wake wa Washington DC imewasiliana na maafisa wa Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Mauaji *(Homicide Section)* huko Detroit kwa ajili ya kupata maendeleo ya uchunguzi wa vifo hivyo. Kwa mujibu wa taarifa ya maafisa upelelezi hao wa Detroit, hadi sasa hakuna aliyekwisha kamatwa au kufikishwa mahamani kwa kuhusika na mauaji hayo na uchunguzi bado unaendelea. Watuhumiwa mbalimbali wamekwisha hojiwa ili kubaini kuhusika au kutohusika kwao na mauaji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Upelelezi wa Kesi za Mauaji ya Detroit, imeeleza ugumu wa kuelezea kwa kina ni hatua gani haswa waliyofikia kwa sasa, kwani hali hiyo inaweza kuvuruga uchunguzi wao. Hata hivyo wameahidi kutoa taarifa ya jumla ambayo itagusia hatua iliyokwishafikiwa katika uchunguzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa kwa kuliuliza swali hili ambalo linagusa mioyo ya Watanzania, hasa familia mbili za Mazula na Nkya ambazo tunazidi kuzipa pole na tunaziomba zivute subira.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwa kuwa kitendo hiki walichofanyiwa raia wenzetu ugenini ni kitendo cha ukatili. Je, Serikali yetu ina msimamo gani wa kukemea kutoa tamko lolote kuhusu kitendo hicho walichofanyiwa raia wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. SEIF ALI IDD):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia njia za kidemokrasia tumewasiliana na Serikali ya Marekani kuelezea kusikitishwa kwetu kwa

kitendo cha mauaji haya na kuhimiza kwamba uchunguzi uendelee kwa haraka jambo ambalo tunalifanya na tunaendelea kulifanya hadi sasa.

Na. 53

**Hitaji la Usafiri wa Treni Tanga- Moshi**

**MHE. NURU A. BAFADHILI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kulikuwa na usafiri wa treni toka Tanga-Moshi iliyoanza safari zake kila siku asubuhi kuelekea Moshi toka Tanga; na kwa kuwa, usafiri huo uliwasaidia wakazi wa Wilaya ya Tanga, Muheza na Korogwe, kufanya shughuli zao za kilimo na biashara:-

(a) Je, ni lini Serikalli itarudisha huduma hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa usafiri huo utawasaidia wanafunzi wanaosoma Sekondari za mbali na ambao asubuhi wanaposafiri kwenda shule na kurudi jioni wananyanyasika katika mabasi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Moja ya hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kukamilisha zoezi la kukodisha Shirika la Reli Tanzania kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri wa abiria na mizigo. Zoezi hili lillikamilika tarehe 1 Oktoba, 2007 ambapo mkodishwaji (*RITES Consortium*) kutoka India ambaye alishinda zabuni ya uendeshaji wa Shirila la Reli Tanzania alikabidhiwa rasmi kuliendesha Shirika.

Ni kweli ilikuwepo huduma hiyo kati ya Tanga na Moshi lakini ilisitishwa kutokana na upungufu na uchakavu wa injini na mabehewa na hali ya ushindani mkubwa wa usafiri kwa njia ya barabara kati ya Tanga na Moshi. *(Makofi)*

Hata hivyo, uendeshaji wa shughuli za usafirishaji ni jukumu la mwekezaji ambaye kwa sasa kipaumbele chake ni kurejesha huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo uanzie Dar es Salaam badala ya kuanzia Dodoma baada ya kufanyia ukarabati mkubwa injini na mabehewa, kukodisha injini na mabehewa toka nje na kununua injini na mabehewa mengine mapya huduma hiyo inaweza ikarejeshwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua wazi umuhimu wa kuwepo kwa huduma ya usafirishaji wa abiria kwa njia ya reli kati ya Miji ya Tanga na Moshi ikiwa ni pamoja na umuhimu wa huduma hiyo kwa usafiri wa wanafunzi kama alivyobainisha Mheshimiwa Mbunge.

Pamoja na kutambua hilo, urejeshaji wa huduma za usafiri wa reli katika mtandao mzima wa reli utatekelezwa hatua kwa hatua kwa kuzingatia tathmini itakayofanywa juu ya mahitaji halisi.

Kwa kuanzia kipaumbele kwa sasa ni kurudisha safari za treni ili zianzie Dar es Salaam badala ya Dodoma mara mbili kwa wiki na nafurahi kulitangazia Bunge lako tukufu kwamba jana tarehe 1 Novemba, 2007 shughuli hiyo imeanza rasmi.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza, kwa kuwa wakopeshwaji hao ambao wameashaanza shughuli zao za usafiri kuanzia Dar es Salaam kuelekea Dodoma.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashawishi wakopeshwaji hao kuanza safari hizo hizo tena kwa Tanga kuelekea Muhenza kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi ambao wanasoma katika shule Kange, Muhenza, Kongwe, Maweni ambao wananyanyasika katika dala dala na usafiri huo ungeweza kuwasaidia ili kupunguza manyanyasiko?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba watafanya tathimini ya hali halisi ya soko itakavyokuwa. Lakini labda la msingi sasa hivi ni kuwashawishi wenye mabasi kuacha huduma ya kunyanyasa kwa sababu usafiri kati ya Tanga na Muhenza ni mwepesi kwa barabara kuliko kwa reli.

Na. 54

**Ukarabati wa Bandari ya Kilwa Masoko**

**MHE. HASNAIN GULAMBAS DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Serikali ya Norway ilikuwa na mpango wa kukarabati Bandari ya Kilwa Masoko:

Je, mradi huo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulambas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Ukarabati wa Bandari ya Kilwa Masoko chini ya ufadhili wa Serikali ya Norway, ulikamilika mwanzoni mwa mwaka 1980 na kuiwezesha Bandari hiyo kuhudumia meli za mwambao, hususan meli za iliyokuwa Kampuni ya Meli Mwambao *(Tanzania Coastal Shipping Line (TACOSHILI*), iliyokuwepo wakati huo. Kwa Bandari ya Kilwa Masoko ina miundombinu inayokidhi mahitaji ya shehena na vyombo vya usafiri wa majini vinavyotia nanga katika Bandari hiyo, ikiwa ni pamoja na gati dogo na ghala la shehena lenye mita za mraba 297.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*), imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya matengenezo muhimu ya miundombinu ya Bandari ya Kilwa Masoko ili iweze kuendelea kuhudumia vyombo vya usafiri wa majini vinavyotia nanga katika Bandari hiyo kwa usalama.

Aidha, Serikali kuptia Mamlaka ya Usimaizi wa Bandari imepanga kufanya utafiti wenye lengo la kubainisha mahitaji ya kuboresha Bandari ya Kilwa Masoko na kuifanya kuwa ya Bandari ya kisasa. Utafiti huu umepangwa kuanza Januari 2008 na kukamilika mwishoni mwa 2008. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii na swali moja la nyongeza Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha bandari ya Kilwa Masoko inapokea mizigo mikubwa mikubwa na midogo midogo kama ile ya Tanga ili kupunguza msongamano uliokuwa katika bandari ya Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Dewji hivi sasa bandari ya Kilwa inafanya kazi chini ya kiwango kilichopangwa na kwamba inayo nafasi ya kubeba mizigo mizito. Sasa ni muhimu tu kumwomba Mheshimiwa Mbunge awashajiishe watu wake waweze kuitumia bandari ya Kilwa ipasavyo.

Lakini nimfahmishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tunayo nia ya kuitengeneza bandari hii ili iweze kusafirisha kwa vizuri zaidi masuala yale ya jasi ambayo yanachimbwa kule ambayo yanakwenda Msumbiji na ambayo yanatumika katika sementi ya Twiga kwa maana hiyo tupo pamoja katika kuboresha bandari hii na kila mwezi tunatumia 1,100,000 kwa ajili ya uendeshaji. Lakini mapato ni milioni 5 kwa mwaka.

Na. 55

**Matengenezo ya Barabara ya Mbalizi Mkwajuni – Makongolosi**

**MHE. VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ya kuanza kuitengeneza barabara ya Mbalizi – Mkwajuni – Makongolosi kwa kiwango cha changarawe bado haijaanza kutekelezwa na sasa inakaribia miaka miwili tangu ahadi hiyo itolewe, na kwa kuwa hali ya barabara hiyo inazidi kuwa mbaya. Je, Serikali inawapa matumaini gani wananchi wa Jimbo la Songwe kwa kutamka ni lini kazi hiyo itaanza kutekelezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kweli hilo jina la katikati ni kiboko limenishinda hapa. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Jimbo la Songwe, kama ifuatavyo:-

Barabara ya Mbalizi – Mkwajuni – Makongolosi yenye urefu wa kilometa 116.6 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Mbeya. Kwa sasa sehemu kubwa ya barabara hiyo ya changarawe pamoja na udongo, hivyo nyakati za mvua, baadhi ya sehemu hupitika kwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhaba wa fedha, ni kweli Serikali haijaweza kujenga barabara yote ya Mbalizi – Mkwajuni – Makongolosi kwa kiwango cha changarawe, ambapo kiasi cha fedha zilizotakiwa ni shilingi 2.915.

Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba barabara hiyo inaendelea kupitika kwa mwaka mzima, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

- Kati ya mwaka 2002/2003 hadi 2006/2007, barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo mbalimbali kwa gharama ya shilingi 687,934,540. Kati ya fedha hizo, shilingi 140 milioni zilitumika kuanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa kujenga kilometa 1.5 kuanzia Mbalizi mjini.

- Kwa mwaka huu wa fedha (2007/2008), jumla ya shilingi 677,229,000 zimetengwa ili kugharamia matengenezo mbalimbali katika barabara hiyo kama ifuatavyo:-

    - Kuendeleza ujenzi wa lami kwa kilometa 4.5 kwa gharama ya Shs. 450 milioni.
    - Matengenezo ya kawaida – Shs. 136,164,000.
    - Matengenezo ya sehemu korofi – Shs. 10,065,000.
    - Matengenezo ya madaraja – Shs. 81,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili barabara yote hiyo iweze kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe kama ilivyoahidiwa.

**MHE. VICTOR KILASILE MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa inafahamika wazi kwamba tatizo kubwa katika ukarabati wa barabara za changarawe ni makandarasi kutokuweka mifereji huku wakijua kwamba adui mkubwa wa barabara ni maji. Kwa hiyo, inabidi barabara itengenezwe kila mwaka na kuharibu hela za wananchi. Je, Wizara inasemaje kuhusu fedha ilizotenga kwa ajili ya kuikarabati barabara hiyo na barabara zote za Mkoani Mbeya?

(b) Kwa upande mwingine wa barabara hiyo hiyo, kutoka Mbeya, Chunya, Makongorosi, kwa kweli napenda niishukuru sana Serikali, Wizara ya Miundombini kwa kuanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kuanzia mwezi uliopita nawashukuru sana.

Katika ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu aliwaahidi wananchi wa Chunya kwamba sehemu iliyobaki ya barabara hiyo kutoka Lwanjilo - Chunya – Makongorosi itawekwa katika vipande viwili mwaka ujao na kwa kuwa inabidi kuwepo na hesabu za kutosha kabla ya kuingia kwenye Bajeti mwaka ujao. Je, Wizara inasemaje kuhusu kutangaza *tender* kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kutoka Lwanjilo – Chunya- Makongorosi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ili barabara iweze kudumu ni vema ikawa na mifereji ambayo inapitisha maji. lakini vile vile ni kweli kwamba kutokana na uhaba wa fedha wakati mwingine kujenga mifereji inayokidhi haja hiyo inakuwa hakuna.

Kwa maana hiyo, mkandarasi hutakiwa kuinua tuta la barabara ili maji yaweze kupita kwa urahisi. Kwa hiyo, kwa kweli wakati mwingine makosa wala si ya mkandarasi, lakini makosa ni matatizo yanayotokana na uhaba wa fedha ambayo hayakidhi kuweka mifereji inayotosheleza na kujenga barabara hiyo.

Lakini ni vema pale ambapo mifereji haijengwi kwa kiwango hicho basi tuta la barabara liweze kuinuka na maji yaweza kupita kwa urahisi. Hilo linazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi ni kweli kwamba ahadi iliyotolewa mwakani ya kuendelea kujenga barabara hiyo iko pale pale. Lakini utaratibu wa kutangaza ukandarasi wa kujenga barabara ni kwamba mpaka fedha ziwe zimefika mkononi kwa maana ya kuidhinishwa na Bunge. Kabla ya Bunge kuidhinisha Bajeti hatuwezi kuanza kutangaza ujenzi huo. Hivyo basi tusubiri mpaka mwakani wakati Bajeti itakapotangazwa na baada ya kuona fedha zimeidhinishwa

na Bunge ukandarasi huo utatangazwa ili kazi hiyo iendelee kama ilivyoahidiwa na Serikali.

Na. 56

**Tatizo la Ndege Waharibifu**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ndege waharibifu wameendelea kuwasumbua wananchi wengi katika Jimbo la Singida Kusini hasa vijiji vya Mlandala, Ighombwe, Masweya, Minyuhe, Msosa na Mtunduru kiasi kwamba, kila wanacholima kinaliwa na ndege hao na kusababisha njaa na umaskini; na kwa kuwa, sasa wananchi hao wamekata tama na kuona kuwa hawana sababu ya kuendelea kulima mazao ya chakula na yale ya biashara:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi hawa ikizingatiwa kuwa, suala hili lilishaletwa Bungeni mara nyingi lakini bado halijapatiwa ufumbuzi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Jimbo la Singida Kusini, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege wanaosumbua wakulima katika maeneo yaliyotajwa wanajulikana kwa jina la Kasuku wa Kijani au kwa Kiingereza *Fischer's Love Bird*. Wizara yangu ilifanya uchunguzi wa kina na kubaini Desemba mwaka 2002. Wizara yangu ilifanya uchunguzi wa kina na kubaini kuwa vijiji 11 katika Wilaya ya Singida na vijiji 6 katika Wilaya ya Iramba vinaathirika na mashambulizi ya ndege hawa.

Hapo awali ndege aina ya kasuku wa kijani walikuwa wanavunwa na kuuza nchi za nje lakini mwaka wa 1992 biashara ya ndege hawa iliwekewa kuzuizi. Kizuizi hiki kilipunguza uvunaji wa ndege hawa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliomba na kupatiwa kibali cha udhibiti kwa mujibu wa Sheria ya Kuhifadhi Wanyama Pori Namba 12 ya 1974 ili kupunguza idadi ya ndege hao. Wizara ilifanya kazi ya udhibiti kwa miaka miwili mfululizo yaani mwaka wa 2003 na 2004. Udhibiti kwa kutumia viuatilifu haukuwa na mafanikio kutokana na uwezo wa Kasuku kujificha chini ya mimea na kutofikiwa na dawa inaponyunyizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilifanya mkutano tarehe 30/4/2004 Mjini Singida wa kuandaa upya mkakati wa kudhibiti ndege hawa. Mkutano huu uliwajumuisha wataalam wa Wizara yangu na Halmashauri za Wilaya ya Singida na

Iramba. Maamuzi ya kikao hiki yalikuwa kwamba Kasuku hawa wanadhibitika kwa ufanisi zaidi kwa kuwatega kwa nyavu na ulimbo.

Katika kuhamasisha utekelezaji wa mkakati mpya wa udhibiti Wizara yangu ilitoa mafunzo kwa wadau 120 wakiwemo wakulima 91, Maafisa Ugani 12 na viongozi mbalimbali kutoka Kata za Wilaya ya Singida Vijijini, juu ya namna ya kutumia mbinu za kuwanasa ndege hao kwa nyavu na ulimbo kwa nia ya kuwatumia kama chakula. Aidha, Wizara yangu iligawa kwa wakulima nyavu 20 na kilo 20 za ulimbo ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa naomba kwa ufupi nijibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu unaotokana na visumbufu vya mazao katika nchi hii ni mkubwa. Kwa mfano, inakadiriwa kuwa ndege wa aina ya Kasuku wa kijani peke yake wasipodhibitiwa wanaweza kuharibu wastani wa asilimia 70% ya mazao wakati *Quelea quelea* nao wanaweza kuharibu hata asilimia 80% ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu umeonyesha kuwa udhibiti wa kasuku kwa kuwavuna kwa ajili ya kuwala peke yake ni mbinu ambayo haina motisha wa kutosha kuwafanya wakulima kuendeleza juhudi za kupunguza idadi ya ndege hao. Aidha, imebainika kuwa kuwavuna ndege hao kwa ajali ya kuwauza nje ya nchi na kujipatia kipato ni njia pekee ya kuwahamasisha wakulima kuwavuna kwa wingi na hatimaye kupunguza idadi yao kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya kuzuia kuwauza nje ya nchi.

Hivi sasa, Wizara ya Maliasili na Utalii iko kwenye hatua za mwisho za mchakato utakaowezesha ndege hao kuanza kuuzwa nje tena. Wakati ndege hao wanatafutiwa soko, Serikali inaendelea kuwashawishi wakulima kutumia mbinu shirikishi. Aidha, fursa zilizopo katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) kuhusu kupambana na visumbufu vya mimea zitatumika ikiwa ni pamoja na uwezeshaji wa wakulima kuwa na mbinu za kupambana na ndege waharibifu kupitia katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Wizara yangu kupitia Kitengo cha Afya ya Mimea, italiangalia upya tatizo hili la Kasuku na kulipatia ufumbuzi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jitihada kubwa alizofanya za kujibu swali hili. Pamoja na hayo naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri katika maelezo yake kwamba uharibifu unaofanywa na ndege hawa wa Kasuku na wale wa *Quelea quelea* ni kati ya asilimia 70 na asilimia 80 kitu ambacho ni uharibifu mkubwa sana. Na kwa kuwa Wizara ya mali asili wameahidi toka mwaka 2003 kwamba watatafuta soko ambako ndege hawa wa Kasuku watauzwe huko nchi za nje na mpaka leo halijamalizika.

Je, ningependa kujua mchakato huu unamalizika lini ili nikitoka hapa nikawape majibu wananchi hawa ambao wamekata tamaa ya kulima kutokana na tatizo hili?

(b) Kwa sababu kwa maelezo hayo ambayo Mheshimiwa Waziri ameeleza na wa umuhimu taifa hili na wananchi hawa ni kukata tamaa ya kuendelea kulima. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuja Singida nimtembeze katika vijiji vyote hivi ili kufufua matumaini ya wananchi kuendelea na kilimo na lini yuko tayari kuja? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mohamed Missanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi Wizara ya Maliasili inakaribia sasa kukamilisha huo mchakato na siwezi nikasema tarehe ni lini, lakini nataka nimhakikishie kwamba mchakato huo unakaribia kukamilika na mara tu ukishakamilika basi hatua zingine zitafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati tumezuia hawa ndege kuuzwa nchi za nje kulikuwa na tatizo lililojitokeza kwa sababu utaratibu uliokuwa unatumika huko nyuma ulisababisha ndege hawa kuharibika na kufa pale Nairobi baada ya kukosa usafiri.

Kwa hiyo, Wizara iliagiza kwamba kwanza tusimamishe na iliagiza *conventional on integrated trade, on integrated species of world Fauna and Flora*. Tatizo hili limefikia mahali pake linapewa ufumbuzi. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwaliko Mheshimiwa Mbunge, naomba nimwarifu kwamba mara baada ya Bunge, nitakuwa na utaratibu wa kutembelea Mkoa wa Singida na kwa hiyo, nitakuja. Kama si mimi basi ni Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu atakuja. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongezea majibu mazuri sana ya Naibu Waziri mwenzangu kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Missanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kufanya masahihisho kwa jina la ndege anayesemwa kuwa ni Kasuku Manjano.

Ndege huyu jina halisi na sahihi la Kiswahili Quela Manjano kwa jina la kingereza ni *fishers love bird* ambao ni kweli wanapatikana Mkoani Singida na mikoa

mingi. Ndege huyu analindwa na mkataba wa Kimataifa wa kulinda viumbe na mimea adimu duniani.

Kwa hiyo, mchakato wa kuruhusu kuuza ni lazima uzingatie mkataba huu ambao Tanzania ni mwanachama. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya nyongeza na hasa kutupa jina sahihi la huyo ndege. Waheshimiwa Wabunge, tumebakiwa na dakika kama tatu, naomba tumalizie swali lililobakia.

Ninaomba nimwite sasa Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, ili aweze kuuliza swali lake linaloelekezwa kwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Na. 57

**Mkutano wa Kimataifa Juu ya Vijana Kupata Uhuru wa Kutoa Maoni**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, tarehe 26/3/2007 kulifanyika Mkutano wa Kimataifa juu ya vijana wa nchi husika kupewa uwezo wa kuanzisha vipindi vyao kwenye vyombo vya habari vya nchi husika ili kuwawezesha kuwa na uhuru wa kutoa maoni yao mbalimbali kwenye maendeleo na Tanzania ilipeleka vijana 13 kuhudhuria Mkutano huo mkubwa:-

(a) Je, ni vijana kutoka Mikoa gani walioshiriki na ni vigezo gani vilitumika kuwapata?

(b) Je, ni vijana wangapi wenye uwezo ambao wanatarajia kutoa elimu walioipata katika Mkutano huo kwa Mikoa mingine iliyokuwa haikupata fursa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO(MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu**:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, kwa uangalifu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya vijana kumi na nne (14) kutoka katika Mikoa ya Dar es Salaam na Kigoma walishiriki katika Mkutano huo. Vigezo ambavyo vilitumika kuwapata vijana hao ni kama ifuatavyo:-

Kigezo cha kwanza ilikuwa awe umri chini ya miaka kumi na nane.Kigezo cha pili ilikuwa ni uelewa wa kuwasilisha taarifa (*Presentation*) kwa watu bila woga. Kigezo cha Tatu ilikuwa ni uwezo wa kuhoji (*interview*) na pia kusoma kwa ufasaha. Kigezo cha nne, ilikuwa ni uwezo wa kutumia mtandao (*website*). Kigezo cha tano, ilikuwa awe ameshiriki katika mafunzo kuhusiana na mawasiliano yaliyoandaliwa na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*).

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wote walioshiriki katika Mkutano huo wanao uwezo wa kutoa elimu kwa vijana wanzao, uwezo wa kutoa elimu kwa vijana walio katika Mikoa mingine ambayo haikupata fursa ya kupeleka vijana wake kwenye mkutano huo nchini Afrika Kusini. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa nini iwe Dar es Salaam na Kagera, ni vigezo gani au ni usaili gani uliofanywa na nani alisimamia usaili huu hadi wakapatikana hawa 14 kutoka katika Mikoa miwili aliyoitaja?

(b) Kwa sababu Serikali hivi sasa zote mbili vyombo vyake vina ushirikiano mkubwa TVT, TVZ Zanzibar, *Radio Tanzania,* Sauti ya Tanzania Zanzibar pamoja na Radio Uhuru hivi Mheshimiwa Waziri hakuona kwamba kuna sababu basi katika kikao hiki angalau vijana kutoka katika vyombo hivyo upande wa pili wa Muungano wakapewa nafasi japo vijana wawili ndiyo sababu ilipelekea hakuna kijana hata mmoja?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MICHEZO NA UTAMADUNI (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili madogo ya Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kama ifuatavyo:-

Kwanza, nikiri kwamba mchakato huu haukuandaliwa na Wizara yetu bali ulifanywa na wenyewe *UNICEF* wakishirikisha Mikoa mbalimbali. Kwa hiyo, Wizara yetu kama Wizara Mama inayoshughulikia vyombo vya habari, haikushirikishwa katika jambo hili na hii ni matokeo ya Sheria yetu ile ya mwaka 2003 ambayo inatoa uhuru kwa vyombo mbalimbali kuwekeza katika sekta ya habari bila mipaka yoyote. Wilaya nyingi sana zilituma maombi kwa mfano Wilaya ya Temeke, Mafia, Bagamoyo, Kilombero, Kisarawe, Hai, Ngara, Mbarali na hata Makete lakini hawakufanikiwa kwa vigezo vilivyowekwa na ndugu zetu wa *UNICEF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli kuna uhusiano wa karibu sana kati ya vyombo vyetu vya *TVT, TVZ,* Radio Uhuru na vyombo vingine lakini katika mchakato huu havikuweza kushinda ili kuviwezesha kwenda Afrika Kusini.

Kwa hiyo, ndugu yangu Hafidh Ali Tahir niseme tu kwamba suala hili lingekuwa limepitia kwetu kuna mambo ambayo tungeyazingatia kama anavyosema vyombo vya upande wa pili wa Muungano na tumekuwa tukilizingatia sana suala hili. Mimi mwenyewe ni hivi majuzi tu nilifanya safari ya kwenda nchi za nje kwenye suala hili la *broadcast* na tumeshirikisha wenzetu wa *TVZ*. Kwa hiyo, suala hilo tunalifahamu sana lakini niseme tena kwamba mchakato huu ulikuwa nje ya utaratibu wa Wizara na uliratibiwa na wenzetu wa *UNICEF*. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali kimekwisha na maswali yote ambayo tulikuwa nayo hapa Mezani kwa siku hii ya leo tumeweza kuyakamilisha kwa maana ya kuulizwa na kujibiwa. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu mpaka tumeweza kumaliza kazi hii ya maswali.

Sasa, kabla hatujaendelea katika agenda nyingine ya kikao chetu cha leo, ninaomba nitoe matangazo ambayo yapo katika Meza ya Mheshimiwa Spika. Kwanza, naomba nitoe tangazo la Mheshimiwa John M. Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, anawaarifu Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kwamba kutakuwa na kikao muhimu leo tarehe 2/11/2007 saa saba mchana katika chumba namba 231 jengo la utawala, ghorofa ya pili. Wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria kikao hicho bila kukosa.

Tangazo la pili limeletwa Mezani na Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika ameniomba niwatakie kila la kheri Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM wanaogombea Ujumbe wa *NEC* katika Mkutano Mkuu wa CCM utakaoanza tarehe 3/11/2007. Mheshimiwa Spika anamwomba Mwenyezi Mungu awape ushindi wa kishindo katika uchaguzi huo ambao utakwenda kufanyika hapo kesho.

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tunawasiliana hapa na Kamati yetu ya Ufundi inayosimamia mashindano ya michezo, nadhani Kamati ile nayo ingeombwa kufanya kazi zake ili ushindi upatikane kama inavyofanya kwenye michezo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine la Kamati linatoka kwa Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa watakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 2/11/2007, saa saba mchana katika ukumbi namba 219, ghorofa ya kwanza, katika jengo la utawala. Wajumbe wote wa Kamati hiyo wanaombwa kuhudhuria katika kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo taarifa nyingine tena ya kikao. Nimeombwa na Katibu wa *TWPG* (Chama cha Wabunge Wanawake), Mheshimiwa Eliatta Namdumpe Switi, ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wanachama wote wa *Tanzania Women Parliamentary Group (TWPG)* kuwa leo tarehe 2/11/2007 kutakuwa na kikao

kifupi sana kuzungumzia masuala ya chama chao kuanzia saa 4:30 asubuhi, nafikiri itakuwa saa 7:00 mchana kwa sababu vikao vya namna hii vyote vinatakiwa vifanyika saa 7:00 mchana, katika ukumbi wa Pius Msekwa ili kuwapa nafasi Wanawake Wajumbe wa Kamati zilizotajwa hapa juu washiriki vikao vya Kamati kwanza. Kwa hiyo, ninaomba tukutane saa 7:00 mchana wanawake wote Wajumbe wa *TWPG* katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Agenda za kikao hicho zimeshaandaliwa na mtapatiwa kwenye kikao hicho, ninazo hapa lakini nyingi zinaonekana ni siri siwezi kuzisema.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Kaimu Kiongozi wa Upinzani Bungeni, ameniomba nitoe taarifa rasmi kwamba leo baada ya muda si mrefu sana atakuwa safarini kikazi Dar es Salaam lakini atakapokuwa hayupo Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, msaidizi wa *Chief Whip* wa Upinzani ndiye atakayekuwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa muda huo wote mpaka atakaporejea tena siku ya Jumapili katika shughuli za Bunge. Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya kwa kushika Kiti hicho kwa muda mfupi. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninaendelea na matangazo ya wageni ambao wako katika ukumbi wetu wa Bunge kwa siku hii ya leo. Tunafurahi wageni wetu leo ni wengi, kwa kweli tunawakaribisha sana na nadhani itabidi niwataje kwa makundi ili tuweze kuendelea na agenda nyingine ili tuzimalize kwa muda tulionao.*(Makofi)*

Kwanza, naomba nitambue uwepo wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wapo kwenye *Speakers Gallery*. Wa kwanza ni Mheshimiwa Salmin Awadhi, karibu sana Mheshimiwa Salmin Awadhi. Wa pili ni Mheshimiwa Ali Suleiman, wa tatu ni Mheshimiwa Ramadhan Pandu, karibuni sana. Hao wote ni wageni wa Mheshimiwa Mohammed Amour Chombon ambao wamekuja kwenye shughuli za Chama lakini pia wamekuja kutembelea Bunge. Karibuni sana, tunafurahi kuwa nanyi. *(Makofi*)

Lakini vilevile nimeombwa na Mheshimiwa Mwaka A. Ramadhan nimtambulishe Mheshimiwa Fuaiba Kisasi na yeye yupo pale mbele, karibu sana Mheshimiwa Fuaiba. Tunafurahi kuwaona wenzetu wa Baraza la Wawakilishi mmekuja kutuunga mkono katika siku hii, karibuni sana. *(Makofi)*

Nadhani tunao wengine pale basi na wao tunawakaribisha, tutaendelea kuwatambulisha kama majina yao yataletwa katika Meza yetu.

Nimeombwa na Mheshimiwa Basil P. Mramba niwatambulishe wageni wake ambao ni Mheshimiwa Anthony Tesha, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, karibu sana Mheshimiwa Tesha. Mheshimiwa Justin Masika ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Rombo, Mheshimiwa Flavian Marandu ambaye ni Diwani wa Halmashauri ya Rombo. Karibuni sana kwenye shughuli zetu za Bunge na ndani ya Ukumbi wa Bunge. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa na Capt. George Huruma Mkuchika kwa niaba ya Wabunge wote wa Mtwara, niwatambue wageni wao wanaoongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa na mkewe, Mwenyekiti huyo anaitwa Mheshimiwa Alhaj Dadi Hamis. Naomba wasimame pamoja na wageni wote kutoka Mtwara. Karibuni na ninaomba msimame tuwafahamu. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni 15 kutoka Kata mbalimbali za Jimbo la Iramba Magharibi wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya. Tafadhali Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya na wageni hao naomba msimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahiri niwatambulishe kwenu wageni wake kutoka *Ward* ya Tomondo Jimbo la Diwani, wanaongozwa na Katibu wa *Ward* hiyo Ndugu Cyprian. Karibuni sana na ninaomba msimame ili tuwatambue. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia mgeni wa Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe naye si mwingine ni Mbunge Mstaafu Semindu Pawa, Mbunge wa zamani wa Jimbo la Morogoro. Ooh! Semindu Pawa naye Mtera. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia nimtambulishe mgeni mwingine Mheshimiwa Charles Kagonja ambaye ni Mbunge wa zamani wa Jimbo la Mlalo. (*Makofi*)

Nimeombwa niwatambulishe wageni wa Mheshimiwa William M. Ngeleja, wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Uandishi wa Habari *Royal College* cha Dar es Salaam wakiongozwa na Rais wa Chuo na Mwalimu Mkuu, karibuni sana. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Issa Kassim Issa, yupo Bwana Yusuph Omar Chunda, Mkurugenzi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar, Ndugu Juma Mohamed, Mwandishi wa Gazeti la Mtanzania, yupo Bwana Khatib Suleiman, Mwandishi wa Gazeti la Uhuru na Mzalendo, yupo Bwana Maulid Othman, Mpiga Picha wa Gazeti la Zanzibar Leo. Karibuni sana na shughuli zetu hizi naamini mtazitangaza mpaka huko Zanzibar. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa na Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman niwatambulishe wageni wake ambao ni Bwana Ramadhan Nyonje Pandu, Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni lakini wote tunakumbuka Bwana Ramadhani alishawahi kuwa Mbunge wa Jimbo hili kipindi kilichopita. *(Makofi*)

Naomba nimtambulishe mgeni wa Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, Bwana Ali Suleiman Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Kazumali Malilo Simba wa Yuda wa Masasi, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Masasi, karibu sana Mwenyekiti wa Chama na ndugu Lydia Katibu wa Wilaya ya Masasi na Wajumbe wa Mkutano kutoka Masasi, tunaomba msimame kwa pamoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia nitambulishe ujumbe kutoka *Muhimbili University*, wako hapa ndani na wao naomba wasimame na wao naona Mtera.

Naomba nimtambulishe mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Khamis Jabir Makame ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Jimbo la Mtoni na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar. Ooh na yeye naona Mtera.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nimtambulishe mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Prof. Henry Robert Mgombelo, Mbunge wa zamani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, anao viongozi na wageni wake kutoka Jimboni wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jimbo, Ndugu Juma Makame Mussa. Naomba wote kwa pamoja wasimame. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wa Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed na wao wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jimbo la Ziwani, Kusini Pemba. Naomba wote wasimame wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jimbo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, naye ana wageni wake wakiongozwa na Katibu wa Jimbo na wakereketwa wengine wote na Katibu, naomba wote wasimame kwa ujumla wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kilontsi Muhama Mporogomyi, anao wageni wake Bwana na Bibi Ruts wafanyakazi wa *DCT* hapa Dodoma na ni raia wa Uingereza. Naomba na wao wasimame. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo langu la mwisho hapa Mezani linahusu burudani. Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mzee wa *TOT*, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba katika kuelekea shughuli nzito ya kesho ya uchaguzi, anawaomba leo muhudhurie *Kilimani Club* kuanzia saa tatu usiku yeye na kikundi chake cha *TOT* pamoja na *Zanzibar Stars*, watatoa burudani ya nguvu na ninafikiri wagombea watapata nafasi ya kujinadi pia katika shughuli hiyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na wale wengine wa Upinzani, tunaalikwa kwenye burudani hiyo kabambe iliyoandaliwa kwa siku hii ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo matangazo ya wageni yaliyofika Mezani kwangu kabla sijasimama hapa kuyatangaza. Yale majina ambayo yameletwa wakati nimeshaanza shughuli hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtanisamehe kwa sababu ni lazima sasa nifuate utaratibu wa kuendelea na ratiba yetu ya leo. Ahsanteni na sasa tunaendelea na ratiba.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya UKIMWI na UKIMWI wa Mwaka 2007 (*The HIV and AIDS (Prevention and Control) Bill, 2007*)**

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi wa Mwaka 2007 (*The Procurement and Supplies Professionals Board Bill, 2007*)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nitoe salamu zangu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Tunaomba Mwenyezi Mungu aipe familia ya Marehemu moyo wa ujasiri na uvumilivu mkubwa katika kipindi hiki cha majonzi. Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya Marehemu, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya ya utangulizi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Bodi ya Watalaamu wa Ununuzi na Ugavi *(The Procurement Supplies Professionals Board Bill, 2007)* pamoja na marekebisho yaliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge, sasa Usomwe Mara ya Pili. Muswada huu Ulisomwa kwa Mara ya Kwanza Bungeni tarehe 15/08/2007. Madhumuni ya Muswada huu ni kutunga Sheria mpya ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ambayo itafuta Sheria ya Bodi ya Usimamizi wa Vifaa *(National Board of Materials Management)* ya mwaka 1981, Sura ya 179 ya Sheria za Nchi inayotumika hivi sasa ambayo ilitungwa kwa lengo la:-

Kwanza, kusajili wataalam wa ununuzi na ugavi. Pili, kutunza *register* ya wataalam hao na tatu kubuni na kusimamia viwango vya utendaji kazi na nne kuendesha mitihani ya taaluma ya ununuzi na ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Muswada huu, mkazo unawekwa katika kurekebisha vyeo na wasifu wa wataalam wa ununuzi na ugavi ili kupanua wigo na

uwezo wao wa kutekeleza sheria kulingana na matakwa ya sasa ya sekta na pia kukidhi mahitaji ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkazo unawekwa katika kupanua wigo wa kiutendaji na kuongeza viwango vya tozo au faini ili bodi iweze kusimamia vizuri sheria kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Aidha, mkazo unawekwa katika kupanga viwango vya mafunzo, uwezo na kuweka utaratibu wa mwenendo wa wataalam wote wa umma na wasio kuwa wa umma.

Vilevile, Muswada unapanua wigo wa kujumuisha manunuzi ya mikataba ya makandarasi na huduma za kitaalam ambayo haikuwepo kwenye sheria ya sasa ambayo inapendekezwa kufutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umeoanishwa na sheria nyingine zinazoshabihiana mfano Sheria ya Manunuzi ya Umma, Na.21 ya mwaka 2004 hususan kwenye eneo la majina na vyeo vya watendaji wa kazi za ununuzi na sifa za wataalam wanaopaswa kusajiliwa.

Muswada utasaidia kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kuanzisha Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ambayo itapanga viwango vya mafunzo, uwezo wa wahusika na kuweka utaratibu wa mwenendo wa watalaam wote wa umma na wasiokuwa katika sekta ya umma.

Ibara ya 35 ya Muswada inaelezea ulazima wa kuidhinishwa kwa uwekezaji wa fedha za Bodi chini ya Sheria ya *Trustees Investment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Fedha za Umma kuhusu ukaguzi wa mahesabu ya Bodi, utaratibu umeelezwa katika Ibara ya 38 hadi 41 ya Muswada.

Eneo lingine linalooanishwa, ni ajira ya watumishi wa bodi kwamba itazingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 198 ya Sheria za Nchi na suala hili limefafanuliwa zaidi katika Ibara ya 10 ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa Sheria ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi umegawanyika katika sehemu saba na una jedwali moja.

Sehemu ya kwanza, inahusu mambo ya utangulizi ambayo ni jina la sheria yenyewe inayopendekezwa itungwe, matumizi ya sheria na tafsiri ya maneno mbalimbali kama yanavyokusudiwa kutumika kwenye sheria husika. Cheo cha Msajili pia

kinabadilishwa kuwa Mtendaji Mkuu kama ilivyo kwa taasisi nyingine zinazosimamia taaluma kama *NBAA*.

Sehemu ya pili ya Muswada inajumuisha Ibara ya 4 - 10 ambazo zinahusiana na kuanzishwa kwa Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi na majukumu yake, zinahusu pia uteuzi wa Msajili na majukumu yake na wafanyakazi wengine wa Bodi. Ajira ya watumishi wengine wa Bodi itazingatia Sheria ya Utumishi wa Umma. Aidha, sehemu hii inaelezea jinsi ya kukasimu madaraka ya bodi kwa Kamati, kwa Mkurugenzi Mtendaji au mtumishi yeyote wa Bodi hiyo.

Sehemu ya tatu ya Muswada inajumuisha Ibara ya 11 – 23 ambazo kwa ujumla wake zinahusiana na usajili wa wataalam wa ununuzi na ugavi na sifa wanazopaswa kuwa nazo. Sehemu hii vilevile inatoa utaratibu wa watalaamu wa ndani na wa nje na majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji ikiwa ni pamoja na kutangaza kwenye gazeti la Serikali majina ya wataalam wa ununuzi na ugavi wenye sifa hizo. Aidha, sehemu hii inakazia kuwa mtu yeyote atatambulika na kuruhusiwa kufanya kazi ya ununuzi na ugavi endapo tu atakuwa amesajiliwa na Bodi hiyo.

Sehemu ya nne, inajumuisha Ibara ya 24 – 29 zinazohusu udhibiti wa mwenendo wa utaalam wa ununuzi na ugavi kwa kuipa Bodi uwezo wa kuwasimamisha kazi, kuwashusha daraja au cheo au kuwafuta kabisa usajili. Sehemu hii pia inatoa uwezo wa kuwarudisha kwenye Daftari Wataalam wa Ununuzi wa Ugavi waliofutwa baada ya Bodi kuridhika na utendaji wao kuwa umebadilika na kufuata maadili za taaluma zao.

Sehemu ya tano inajumuisha Ibara ya 30 – 33, zinazohusu uanzishaji wa Bodi ya Rufaa na kueleza muundo wake. Sehemu hii vilevile inaelekeza utaratibu wa Bodi ya Rufaa na haki ya kukata rufaa kwa mtu ambaye hatakubaliana na uamuzi uliotolewa na Bodi. Sehemu hii inaipatia Bodi ya Rufaa uwezo sawa kwa maamuzi yake na Mahakama Kuu.

Sehemu ya sita inajumuisha Ibara ya 34 – 41 ambazo zinahusiana na masharti ya fedha kwamba vyanzo vya fedha katika eneo hilo vimeainishwa. Sehemu hii inaipata uwezo Bodi kuwekeza fedha zake na kuazima baada ya kupata kibali cha Waziri mhusika mwenye dhamana ya Bodi hiyo. Zoezi la kuwekeza litafanywa kwa kuzingatia Sheria ya *Trustees Investment* ya mwaka 1967.

Pia katika sehemu hii, Bodi inatakiwa kutayarisha bajeti ya kila mwaka na kuweka na kutunza vitabu vya *Accounts* pamoja na kumbukumbu za Bodi. Vitabu vya fedha vitakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kulingana na Sheria ya Fedha za Umma.

Sehemu ya saba ya Muswada inajumuisha Ibara ya 42 – 51 ambapo kwa ujumla wake vinaweka masharti mbalimbali ambayo yanahusiana na namna ya kushughulikia malalamiko, wajibu wa Wajumbe wa Bodi, utoaji wa ajira kwa watu wasiosajiliwa, ulazima wa kuajiri Watalaamu wa Ununuzi na Ugavi waliosajiliwa, uwezo wa Waziri

kutunga Kanuni, madaraka ya Waziri kumsamehe mtu yeyote kutofuata baadhi ya vifungu vya Sheria hii kwa kushauriwa na Bodi yenyewe. Sehemu hii inafuta Sheria ya Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa ya mwaka 1981.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu una jedwali moja linaloelezea masuala mbalimbali kuhusu Bodi ambayo ni pamoja na mikutano ya Bodi yenyewe, upatikanaji wa Makamu Mwenyekiti, Muundo wa Bodi, Maamuzi ya Bodi na muhtasari wa vikao vya Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kumaliza hotuba yangu, niruhusu nichukue nafasi hii nitoe shukrani zangu za dhati kwa wadau mbalimbali walioshiriki katika kutoa maoni yao wakati wa *public hearing* iliyofanyika mjini Dar es Salaam tarehe 24/10/2007. Maoni na ushauri wao umesaidia kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipoutambua mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kwa ushirikiano wa karibu wakati wa *public hearing* na pia wakati wa kupitia Muswada huu Ibara kwa Ibara katika Mkutano uliofanyika kati ya tarehe 25 -26/10/2007. Uchambuzi wa kina wa Muswada huu uliofanywa na Kamati ya Bunge ya Miundombinu ndiyo uliowezesha Muswada huu uweze kuwasilishwa leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Tunaishukuru Kamati hiyo kwa kutuunga mkono katika Muswada huu. Napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuuandaa kwa ufasaha na umakini mkubwa Muswada huu pamoja na orodha ya marekebisho iliyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Ninawashukuru pia Manaibu Mawaziri wa Wizara yangu Mheshimiwa Dr. Maua Daftari na Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu kwa ushirikiano wao katika kuandaa Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa ninayo heshima ya kuwasilisha Muswada wa Sheria Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (*The Procurement and Supplies Professional Board Bill, 2007*) ambao unapendekeza kufuta sheria iliyopo hivi sasa ijulikanayo kama *The National Board for Materials Management Act* ya mwaka 1981.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kisha liupitishe Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI (K.n.y. MHE. MOHAMED M. MISSANGA) – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi wa mwaka 2007 *(The Procurement and Supplies Professionals Board Bill, 2007)* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na.70(2), Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kutoa salaam zangu za rambirambi kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha Marehemu Salome Joseph Mbatia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto aliyefariki tarehe 24 Oktoba, 2007. Tutamkumbuka Marehemu Salome Mbatia kwa utendaji wake mzuri wa kazi na mchango wake katika Taifa hili. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, napenda kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopata ajali katika maeneo mbalimbali hapa nchini pamoja na wale waliofiwa na wapendwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Tisa wa Bunge, Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi wa mwaka 2007 ambao unafuta Sheria ya Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa (*The National Board for Materials Management Act*), Sura ya 179. Sheria ya Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa inayotumika sasa ilitungwa mwaka 1981 ambayo haikidhi mahitaji ya sasa ya ununuzi na usimamizi wa vifaa. Napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu ilitekeleza kazi hiyo kikamilifu kwa kushirikiana na Waziri wa Miundombinu pamoja na watendaji wa Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 62(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau mbalimbali wanaohusika na Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi wa mwaka 2007 na kupata maoni na mapendekezo yao. Maoni ya wadau hao yaliwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 24 - 25 Oktoba, 2007 katika vikao vilivyofanyika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawapongeza kwa dhati wadau wote kwa ushiriki wao katika kuandaa Muswada huu ambao ni kutoka sekta na taasisi mbalimbali za Kiserikali na zisizo za Kiserikali kama vile Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa *(NBMM),* Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu *(NBAA),* Mamlaka ya Udhibiti wa Zabuni *(PPRA),* Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu *(SUMATRA),* Chuo cha Biashara *(CBE),* Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka *(DAWASA)* na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine walioshiriki ni pamoja na Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA),* Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA),* Chuo cha Uhandisi *(UDSM),* Chama cha Washauri Tanzania *(TACO),* Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA),* Bodi ya Wahandisi *(ERB),* Bodi ya

Makandarasi *(CRB),* Baraza la Taifa la Ujenzi *(NCC),* Shirika la Reli Tanzania *(TRL), Crown Agents, K & Associates Professionals Services Ltd (KAPSEL), Howard Humphreys*, *Lomo Consultants,* pamoja na wengine wengi ambao sitaweza kuwataja lakini kwa namna moja ama nyingine walishiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha Wizara mbalimbali katika maandalizi ya Muswada huu chini ya Wizara ya Miundombinu, Kamati yangu ilishirikisha kikamilifu Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao utawezesha kuwepo kwa sheria mpya itakayokidhi mahitaji yaliyopo katika sekta ya ununuzi na ugavi.

Sheria hii mpya inakusudia kuweka mfumo madhubuti wa usimamizi na utendaji kazi wa Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ambayo itarahisisha utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, Na. 21 ya Mwaka 2004 (*Public Procurement Act No. 21 of 2004*), ambao utaendana na mazingira ya sasa ya soko huru lenye ushindani na mbinu mpya za ununuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii pia itawataka wale wote wenye mali na kipato (*assets and turnover*) zaidi ya Sh.200mil kuhakikisha kuwa shughuli zao za ununuzi na ugavi zinafanywa na watu wenye viwango na taaluma inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Awali ya yote, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kufanya marekebisho ya sheria hii, ambayo yameenda sambamba na sera mpya iliyopo sasa ya Utawala Bora na Sheria ya Manunuzi ya Umma, Na. 21 ya mwaka 2004. Sheria hii inalenga kuleta ufanisi na uadilifu katika utendaji na mwenendo mzima wa Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa kuwa malengo ya Muswada huu ni mazuri kwa manufaa na maslahi ya maendeleo ya Taifa letu, Kamati inashauri Serikali kutoa kipaumbele katika kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ili kuiwezesha Bodi hii kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kumudu gharama za kutoa Elimu kwa vitendo kwa wahitimu wa fani hiyo.

Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Bodi inayoanzishwa, kubuni utaratibu mzuri wa kuwabadilisha wale waliokuwa wakifanya kazi hizi kwa kutumia uzoefu bila kuathiri ajira zao ikiwa ni pamoja na kuwapangia utaratibu wa kujiendeleza. Aidha, Kamati inawashauri wale wote wanaofanya kazi za ununuzi na ugavi kujiendeleza ili waweze kusajiliwa na bodi na hivyo kuendana na matakwa ya sheria hii mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Wizara kwa kushirikiana na Bodi kuharakisha uandaaji wa kanuni ili kuweza kutoa mwongozo na majibu kwa baadhi ya masuala yanayoweza kujitokeza katika utekelezaji wa sheria hii mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwenye sheria hii Ibara ya 18 inayohusu usajili wa wageni hakionyeshi namna ya kuwabana wageni hasa wanaofanya shughuli za ununuzi katika mashirika ya kigeni au Kimataifa, hivyo Kamati inaishauri Wizara kuwa katika kutengeneza kanuni ufafanuzi na utaratibu unaoeleweka ni muhimu ukaelezwa bayana kuhusiana na usajili kwa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuishauri Wizara kwa kushirikiana na Bodi kutoa elimu ya kutosha kwa umma na wadau wote juu ya sheria hii mpya ya wataalamu wa ununuzi na ugavi. Kamati inaikumbusha Wizara kuwa bado ina jukumu la kuisaidia Bodi katika kusimamia na kuratibu mienendo ya ubora wa taaluma za ununuzi na ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa kuwa idadi ya wahitimu wa fani ya ununuzi na ugavi haitoshelezi mahitaji ya Taifa, ambapo mpaka sasa mahitaji ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ni zaidi ya 15,045 kwa ngazi za juu na kati, ambapo mpaka sasa Bodi imeweza kusajili Wataalamu 1,891 tu. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali na sekta binafsi kutoa kipaumbele juu ya kuwaelimisha na kuwaendeleza waajiriwa wao walio katika fani ya ununuzi na ugavi ili kuongeza idadi ya wataalamu na kuzuia ununuzi usio wa kitaalamu na upotevu wa mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** pia Kamati inaishauri Serikali na hata sekta binafsi kuacha kufanya shughuli za ununuzi na ugavi kiholela usiozingatia misingi bora na maadili ya fani kwa kuwatumia watu wasiokuwa na taaluma na badala yake ihakikishe kuwa inaajiri watu wenye taaluma ya ununuzi na ugavi kwa kuwa kuna wahitimu wengi wa fani hii ambao hawana ajira ya kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** vilevile Kamati inaishauri Serikali kuipatia Bodi vifaa na nyenzo za kisasa za kufundishia na zitakazowawezesha kufanya utafiti wa kitaaluma na kutoa ushauri kwa Serikali kwenye maeneo yanayohusu taratibu na sera za ununuzi na ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati inaishauri Bodi kuendeleza jitihada za kupanua huduma za Bodi kufika kwenye sehemu ambazo hazijafikiwa kwa mfano kufungua vituo vya kuendeshea mafunzo au mitihani Mikoani. Kwa sasa huduma hizo zipo kwenye Mikoa michache ya Mbeya, Mwanza, Singida, Tanga, Moshi, Dar es Salaam, Mtwara, Arusha, Dodoma na kituo kilichopo Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge na Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari, Mbunge na Mheshimiwa Dr. Makongoro M. Mahanga, Mbunge, Naibu Mawaziri wa Miundombinu, Ndugu Enos S. Bukuku, Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na Ndugu Omar A. Chambo, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Wataalamu na Watendaji wote wa Wizara hii walioshirikiana na Kamati katika kuandaa na kutoa maelezo ya kina pale yalipohitajika. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalamu wake kwa kutoa ufafanuzi wa vipengele mbalimbali kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati inawashukuru wadau wote niliokwisha wataja hapo awali kwa ushiriki wao katika *"Public Hearing"* na kutoa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia katika kukamilisha na kuuboresha Muswada huu. Kushiriki kwa Wadau hao kumesaidia kufanya kazi ya Kamati kuwa rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu ambao walishiriki kikamilifu katika kuujadili na kuuboresha Muswada huu. Marekebisho yaliyofanyika kama yanavyoonekana katika *Schedule of Amendment* ni ushahidi na kielelezo katika kazi nzuri iliyofanywa na Kamati yangu. Naomba niwatambue kwa majina Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mohammed H. Missanga, Mwenyekiti, Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija S. Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Pascal C. Degera, Mheshimiwa Bakar Faki, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Dr. Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Sigsfrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Mwaka A. Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Hafidh A. Tahir, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi na mimi mwenyewe Mheshimiwa Rosemary Kirigini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Justina M. Shauri, Ndugu Zainab A. Issa na Ndugu Michael Chikokoto, kwa kuweza kuihudumia vema Kamati na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati inaunga mkono kwa dhati kuwasilishwa kwa Muswada huu na kujadiliwa Bungeni. Kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naunga mkono hoja na naomba Waheshimiwa Wabunge wote waujadili na kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, ahsante sana kwa kutoa taarifa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Mohamed Missanga.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani anayehusika na Wizara ya Miundombinu.

**MHE. KHADIJA S. ALLY AL-QASSMY (K.n.y . BAKARI SHAMIS FAKI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA**

**MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii nikaweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni yetu kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuundwa kwa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ya mwaka 2007 (*The Procurement and Supplies Professionals Board Bill,2007*), kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na.43(5)(b)(c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki kifupi, tumepata misiba na maafa kadhaa. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa pole zetu za dhati kwa familia, ndugu na jamaa kwa kifo cha Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge, Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa kufiwa na mama yake mzazi na Mheshimiwa Mustafa Mkulo Mbunge, Naibu Waziri wa Fedha kwa kufiwa na mama yake mzazi pia na wale wote waliofiwa na wapenzi wao.

Aidha, tunatoa pole kwa wale wote waliopata ajali na maafa akiwemo Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mbunge, Mheshimiwa Juma Athuman Kapuya, Mbunge, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mwenyezi Mungu awape nafuu na roho ya ustahimilivu, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumjalia Kiongozi wetu wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa sababu operesheni yake imeenda salama na hali yake inaendelea vizuri. Mwenyezi Mungu amjalie afya njema arudi kuja kuungana nasi kuliendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wa jumla kuhusu madhumuni na sababu za kuanzishwa au kutungwa kwa Muswada huu, Kambi ya Upinzani inaona hii inalenga kuongeza ukubwa wa Serikali kitu ambacho kinaongeza matumizi ya Serikali na kumzidishia mwananchi mzigo wa kodi. Kambi ya Upinzani inaona kuwa malengo yanayokusudiwa na Muswada huu yanaweza kutimizwa kwa uhakika na chombo kingine cha Serikali ambacho kiliundwa kisheria cha *Public Procurement Regulatory Authority (PPRA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa njia rahisi na ambayo haitoongeza matumizi kwa upande wa Serikali na kuongeza mzigo kwa walipa kodi ni kuifanyia marekebisho Sheria ya *PPRA* ya mwaka 2004 ili kukidhi matakwa na malengo ambayo yanaanzisha Sheria ya Uundwaji wa Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni hasa ya kuanzishwa kwa Muswada huu kama ilivyo kwenye Ibara ya 4(1) ni Kuunda Bodi ya Taaluma ya Ununuzi na Ugavi ambayo kwa muonekano wake inatakiwa iwe kama Bodi ya Wanasheria, Madaktari,

Wanamisitu na kadhalika. Kwa hiyo, uanzishwaji wa Bodi hiyo unatakiwa uanzishwe na wao wanataaluma wa taaluma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi kuanzishwa kwa pesa za kodi ya walipa kodi ni kutokutenda haki kwa taaluma zingine kama vile za Wanasheria, Wafamasia, Madaktari na kadhalika kwa kuwa nao wana bodi au jumuiya zao zinazodhibiti nidhamu ya wanataaluma katika fani zao. Tunaomba tupatiwe maelezo ni kwa nini Bodi ya Taaluma hii ipewe kipaumbele zaidi kuliko Bodi za Taaluma zingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ya uhakika kuhusu mambo mawili yafuatayo:-

*(a) Independence* au *autonomy of the Board*

(b) Kazi itakayofanywa na Bodi hii kweli italeta mwamko na kuinua taaluma ya manunuzi na ugavi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo wa jumla kuhusu madhumuni na sababu za uanzishwaji wa sheria hii, naomba kuangalia baadhi ya vifungu ambavyo kwa upande wetu tunadhani vinafanya Muswada huu kukosa sifa za sehemu (a) na (b) hapo juu kwa kuwa mambo yote yaliyoainishwa ndani ya Muswada huu yatakuwa chini ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4(3)(a)(b) na 4(4) na 4(5) vinaonyesha kuwa wajumbe wote wa Bodi wanateuliwa na Serikali kuanzia Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Mheshimiwa Rais na wajumbe wengine wanateuliwa na Mheshimiwa Waziri. Kwa mtazamo wetu ni kuwa Serikali haina utamaduni wa kujidhibiti na mifano mingi ambayo ipo. Kwa kuwa Serikali ndio mhusika mkuu katika ununuzi na ugavi, hivyo ni muhimu chombo ambacho hakina mamlaka ya Kiserikali kihusike na udhibiti wa nidhamu ya watendaji katika taaluma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika uteuzi wa Mheshimiwa Waziri kwa wajumbe wa Bodi, Ibara ya 4(3)(b) kinasema na ninanukuu:-

*"Not less than six nor more than eight other members who shall be appointed by the Minister out of whom half shall be Procurement and Supplies Professionals".*

Swali tunalojiuliza ni je, nusu nyingine ya wajumbe ni kuwa wanaweza kutoka katika kada tofauti na ile ya taaluma ya Ununuzi na Ugavi? Kama ndio hivyo Bodi hiyo kweli itakuwa ni kwa taaluma tajwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa wajumbe wote wawe ni wanataaluma iliyokusudiwa na kama mahitaji ya wajumbe wengine itakuwepo basi wawe ni '*Ex-officio'* au *Co-opted members* kadri watakavyohitaji kwa mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inadhani ingekuwa ni bora kushirikishwa wanataaluma toka kwenye taasisi zinazotoa mafunzo ya ununuzi na ugavi kwenye Bodi hii ili lengo la kudhibiti nidhamu ya kitaaluma liweze kupata ufanisi mzuri. Nidhamu ya kitaaluma haiwezi kudhibitiwa kwa wakufunzi wa taaluma husika kutokuwa na uwezo wa kutoa maamuzi katika taaluma hiyo. Kwa njia hii kutapunguza uwezekano wa msuguano kati ya wanataaluma wa ununuzi na ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mwenyekiti na wajumbe wote wa Bodi wanateuliwa na Viongozi Wakuu wa Serikali na kwa kuwa Serikali ndio chombo kikuu kinachotumia huduma ya taaluma hii ya ununuzi na ugavi, hivyo itakuwa ni bora asasi zingine ziruhusiwe ili ziweze kudhibiti taaluma na nidhamu ya wanataaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 7 inayoelezea kazi za Bodi, katika vifungu vidogo vya (e) na (f), Kambi ya Upinzani inadhani huu sasa ni muda muafaka ambapo bodi iache kusimamia mitihani katika fani hii na badala yake ijihusishe na uwekaji wa viwango vya taaluma zinazotolewa kwa kuweka vigezo vya uanzishwaji wa vyuo vinavyotoa taaluma hii. Hii ni kwa sababu hakuna chombo ambacho kitakuwa kina-*regulate* mitihani inayotolewa na Bodi na mbaya zaidi vyeti vitakavyotolewa na Bodi havitakuwa na ubora wa Kimataifa. Aidha, kwa njia hii kutaondoa mvutano kati ya Bodi na wanaotoa taaluma hii katika vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 17(1) kinachomtaka Mtanzania yeyote ambaye atapata taaluma hiyo nje ya nchi kutokupewa usajili mpaka awe kwenye uangalizi wa mwaka mmoja, Kambi ya Upinzani inadhani sheria hii ingeweka wazi aina ya vyuo ambavyo wahitimu wake watapewa usajili wa uangalizi kwa mwaka mmoja. Tunaamini kuwa ili kuweka kipengele hiki ingekuwa ni bora washirikiane na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwani Wizara hiyo inayo orodha ya vyuo vyote Duniani ambavyo vinatoa elimu yenye ubora unaotambulika Kimataifa. Kinyume na hapo ni kutokuwatendea haki wale wote waliopata fani hiyo katika vyuo bora nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 29(1)(c) inayohusu mtu atakayepatikana na hatia kulingana na utaratibu wa sheria hii, Waziri anapewa mamlaka kutoa adhabu kupitia kwenye kanuni zinazolinda sheria hii. Kambi ya Upinzani inaona hili la kumpa Waziri uwezo wa kutoa adhabu kupitia kwenye kanuni atakazozitengeneza yeye ni bora sheria ingeweka kiwango cha adhabu zenyewe ili kanuni zitakazotengenezwa ziwe katikati ya kiwango kilichosemwa katika sheria. Isitoshe, ni vema kutenganisha mamlaka ya adhabu na ya Waziri ambaye anatakiwa kuwa msimamizi wa Sheria. Kifungu hiki kitaleta mgongano mkubwa wa maslahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 31 inayohusiana na Bodi ya Rufaa, kulingana na mlolongo mzima wa wale wote waliomo katika Bodi hii, ni dhahiri kuwa Bodi haihusishi wale waliomo katika utaratibu wa Kimahakama. Hivyo basi, itakuwa ni bora kama Mwenyekiti wa Bodi hii kuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 32 inayohusu "*Proceedings of Appeals Board*", Kambi ya Upinzani inaona kwa kuwa dhana nzima ya Muswada wenyewe unahusu nidhamu ya taaluma ya ununuzi na ugavi hivyo basi katika mchakato mzima wa Bodi ya Rufaa ni lazima "*Expert Witness*" ahusishwe na ushauri wake uzingatiwe kama ambavyo inatokea katika kesi nyingne zinazohusiana na taaluma, vinginevyo itakuwa ina ukiukwaji wa haki za msingi kwa mrufani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea maoni kutoka Kambi ya Upinzani yaliyowasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa Khadija All Al-Qassmy, naomba sasa nichukue nafasi hii kuwataja kwanza wachangiaji ambao wameshawasilisha maombi yao hapa Mezani kwangu halafu tutaendelea na mjadala wa pamoja. Wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Paschal Degera na wa pili atakuwa Mheshimiwa Herbert James Mntangi, wa tatu atakuwa Mheshimiwa Chacha Wangwe na wa nne atakuwa Mheshimiwa William Shellukindo.

Lakini kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Paschal Degera, naomba nitambue kurudi tena ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa *Chief Whip,* Mheshimiwa Dr. Batilda Burian ambaye alikuwa safarini na amerejea na sasa yupo tena ndani ya ukumbi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Capt. John Chiligati ameachia ile nafasi na amerudi kwenye nafasi yake. Karibu sana Mheshimiwa *Chief Whip*. *(Makofi)*

Baada ya tangazo hili, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Paschal Degera aanze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu na atafuatiwa na Mheshimiwa Herbert James Mntangi.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa asubuhi hii ili niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu wa Sheria ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi wa mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kabla sijaanza kuchangia naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi, kwanza kwa familia, ndugu na jamaa kwa kifo cha Marehemu Salome Joseph Mbatia aliyekuwa Mbunge na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, aliyefariki kwa ajali mbaya tarehe 24 Oktoba, 2007. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliopata matatizo mbalimbali. Wale waliopata ajali, waliopata maradhi na hata waliofiwa, nawapa pole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie maeneo machache. Lakini kwanza ni nitamke *(declare interest)* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu ambayo ilipitia Muswada huu na pili napenda niseme tu kwamba naungana kabisa na maoni ya Kamati ambayo yametolewa na Mjumbe kutoka Kamati hiyo. Aidha, napenda niishukuru sana Serikali kupitia Waziri wa Miundombinu kwa marekebisho mengi ambayo ameyafanya katika Muswada huu kwa lengo la kuuboresha. Jedwali tulilopewa limefanya marekebisho makubwa sana na matokeo yake ni kwamba Muswada wetu umeboreshwa sana , hivi sasa uko katika hali nzuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba nichangie maeneo machache ambayo nimeona yana dosari kidogo, niende katika Muswada wenyewe. Ukiangalia Ibara ya 9(2) inayohusu uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Bodi, napenda niseme kidogo tu kwamba nadhani kuna dosari katika uteuzi ama sifa. Kuna upungufu, sifa za Mtendaji Mkuu wa Bodi hazikutajwa katika Ibara hiyo. Nataka nitoe mfano tu kwamba Ibara hiyo inasomeka kama ifuatavyo: "*The Minister shall appoint Public Officer to be Executive Director* na kuendelea". Mimi nafikiri kuna haja ya kuwa na sifa kidogo pale kwamba atokane na taaluma ambaye anaishughulikia, si kwamba *Public Officer* yeyote. Pia niunganishe katika Muswada wa Wataalamu wa Maabara, hii iliwekwa vizuri sana tulivyopitisha jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirejee tu ile sehemu, Ibara ya 10(1) inasema hivi, *"The Minister shall appoint Health Laboratory Practitioner from the Public Service"*. Nafikiri pale inabaini Mtendaji Mkuu anayetakiwa awe ni wa aina gani, lakini katika Muswada wetu huu haijabaini kwamba huyu Mtendaji Mkuu atakuwa na taaluma gani, haijasema. Inasema tu kwamba awe Mtumishi wa Serikali, nafikiri haitoshi. Naomba kama inawezekana basi Waziri a-*note* sehemu hiyo na ikiwezekana aweze kufanya marekebisho kama si katika Muswada huu basi hata katika kanuni ambazo atatunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende tena Ibara hiyo hiyo, lakini pia 10(4). Naipongeza sana Serikali kwa kufanya mabadiliko makubwa katika Ibara ya 10(4). Awali Muswada ulipendekeza kwamba Mtendaji Mkuu anaweza kuajiriwa kwa kipindi cha miaka minne minne, vipindi viwili tu hata kama Mtendaji huyo angekuwa mzuri namna gani akishafikisha miaka minane basi utumishi wake katika Bodi ungekoma. Lakini sasa Serikali imebaini kwamba kuna dosari. Kwa hiyo, imefanya marekebisho na kuruhusu Mtendaji yeyote ambaye atakuwa na uwezo wa utendaji basi anaweza kuendelea kuteuliwa ili mradi anairidhisha Bodi ama Serikali. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kufanya marekebisho hayo katika ibara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Ibara ya 29 (a) mpaka (c) inazungumzia juu ya makosa, lakini haikuzungumzia juu ya adhabu kuhusu makosa ambayo yatatendwa katika Ibara hiyo, badala yake Muswada unapendekezwa kwamba adhabu itatolewa kupitia kanuni ambazo atatengeneza Waziri, nafikiri hii sio sahihi. Kama makosa yametajwa katika sheria naona ni sahihi au ni vizuri pia adhabu ikatolewa katika sheria

hiyo hiyo badala ya kutolewa kupitia kanuni. Kwa hiyo, napendekeza kwamba Mheshimiwa Waziri angefanya marekebisho na adhabu zingetajwa katika Ibara hiyo kwa sababu siamini kwamba ni vizuri kwenda kutoa adhabu, makosa yake yapo kwenye sheria lakini adhabu inatolewa kupitia Kanuni, nafikiri sio sahihi. Kwa hiyo, napendekeza adhabu zitolewe kupitia Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda nilichangie ni aya ya 47 inayohusu sharti la kuajiri wataalamu wa Ununuzi au Ugavi. Sharti hilo linasema, “kila mtu mwenye mali (*asset*s) ya thamani ya shilingi milioni 200 na biashara kama *turnover* kwa Kiingereza kama ilivyotajwa katika Muswada ya kiwango cha shilingi milioni 100 kwa mwaka atawajibika kwa sheria hii kuajiri mtaalamu wa ununuzi na mtaalamu wa ugavi”.

Maneno yaliyotumika katika Muswada huu “kila mtu” nafikiri sio sahihi, kwa sababu wafanyabiashara wadogo wadogo kwanza kiwango hicho kinachotajwa cha *turnover* ni kidogo sana. Pili, hizo *assets* zinazotajwa ni ndogo sana. Ukimwajibisha kila mmoja aajiri mtaalamu wa Ugavi na Ununuzi nafikiri si sahihi. Labda kama unataka kuniambia kwamba kila Idara ya Serikali ambayo ina kiwango hicho labda waajiri, lakini kila mtu mimi nafikiri tungeangalia ibara hiyo na tuifanyie marekebisho.

Aidha, napendekeza kwamba kiwango hicho cha shilingi milioni 200 na shilingi milioni 100 kingeangaliwa upya kwa sababu viwango hivyo ni vidogo sana na hasa tukizingatia kwamba nchi hii kila siku inapoteza thamani. Kwa hiyo, baada ya miaka miwili mitatu utaona kwamba biashara ya shilingi milioni 100 itakuwa ni ndogo sana na haihitaji kuajiri wataalamu ambao wanaweza kumaliza mtaji wa biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo nimalizie eneo la mwisho. Ukisoma maoni ya Kamati inabaini kwamba wataalaamu wa ununuzi na ugavi nchini ni wachache sana. Hivi sasa waliokwishaandikishwa hawazidi wataalamu 4,000, ni kati ya 3,500 mpaka 4,000. Lakini mahitaji ni 15,000, kwa hiyo, tunayo tofauti kubwa sana ya wataalamu waliopo na wanaohitajika kwa maneno mengine. Ni kwamba nchini hatuna wataalamu wa kutosha wa ununuzi na ugavi. Napendekeza kwamba baada ya Muswada huu kupitishwa basi Serikali ifanye kila linalowezekana kufungua vyuo ama kozi mbalimbali ambazo zinaweza kufunza na kupata wataalamu katika fani hii ya ununuzi na ugavi. Kwa hiyo, katika utendaji wa Serikali basi uangalie ni vyuo gani vitaongezwa ili wataalamu hao waweze kupatikana kwa wingi na kuweza kutosheleza mahitaji, vinginevyo sheria hii haitatekelezeka kwa sababu wataalaamu ni wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na natamka kwamba naunga mkono Muswada huu, ahsante sana. (*Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ili leo niweze kuchangia Muswada huu muhimu wa Sheria ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi wa Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kutoa rambirambi kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama, kwa ndugu na familia ya aliyekuwa Naibu Waziri, Mheshimiwa, Marehemu Salome Mbatia. Sisi watu wa Muheza kifo hiki kimetugusa sana hasa kwa sababu kabla ya kifo hiki kutokea alikuwa katika Wilaya yetu ya Muheza kwa shughuli za kikazi siku chache na hatimaye kifo kikamkuta. Kwa hiyo, watu wa Muheza wanasikitika sana na kwa niaba yao wote tunatuma salamu zetu za rambirambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwape pole wale wote ambao wamepata misiba ya kifamilia, ni wengi lakini tunaomba wote wapate faraja na Mwenyezi Mungu awape subira. Naomba pia kuchukua nafasi hii kuwapa pole ndugu zangu wote ambao wamepata ajali mbalimbali hasa rafiki yangu Mheshimiwa Kapuya, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na vilevile rafiki yangu mpendwa, Mheshimiwa Mudhihir ambaye amepata ajali. Bila shaka Mwenyezi Mungu atawasaidia na maumivu yataendelea kupungua na watakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa na imani kubwa nilipoona Muswada huu umeandaliwa, kwa sababu mbili kubwa. Kwanza, Wizara yenyewe ya Miundombinu ina wataalamu wazuri lakini vilevile inaongozwa na wataalamu. Mheshimiwa Waziri mwenyewe ni mtaalamu ambaye kwa kweli amekuwa akijihusisha sana na mambo ya uandishi wa Miswada na hivyo sikuwa na wasiwasi kuwa ametumia utaalamu wake katika kuhakikisha Muswada huu unakuwa imara.

Vilevile Naibu Waziri wake Mheshimiwa Makongoro Mahanga ni mmoja kati ya waasisi wataalamu wa Bodi iliyokuwepo hapo awali. Ameandikishwa na Bodi ile kama mtaalamu na ametumia utaalamu wake katika kuboresha Muswada huu. Nilipousoma sikuwa na wasiwasi mkubwa, lakini kilichonivutia zaidi niliona jinsi walivyokuwa wakarimu kwa kukubali kufanya marekebisho kusikiliza ushauri wa Kamati ya Miundombinu pamoja na wataalamu wengine na wakakubali kufanya marekebisho katika Muswada huu, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama ili nisaidie kuliwezesha Taifa kufahamu umuhimu wa kuwa na sheria ya namna hii. Kwa upande wangu na naomba Watanzania waelewe kwamba zaidi ya asilimia 90 ya fedha za maendeleo Serikalini matumizi yake yanapitia katika mkondo unaohitaji wataalamu wa aina hiyo. Zaidi ya asilimia kubwa ya fedha za maendeleo, Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa matumizi yake yanahitaji wataalamu wa aina hii. Nitatoa mifano michache tu ili Watanzania pia waelewe umuhimu wa wataalamu hawa unavyohitajika. Hebu tujikumbushe katika ununuzi katika maeneo yafuatayo: ununuzi wa magari yote ya Serikali ni mengi na ya thamani kubwa hivyo anatakiwa mtu mtaalamu aweze kufanya kazi hiyo kununua na kuweza kufahamu tutaweza kununua kwa bei gani itakayokuwa na manufaa kwa Taifa letu. Tujikumbushe

pia ni kiasi gani tunahitaji vifaa kwa ajili ya Ofisi za Serikali, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, fedha zinazotumika pale ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahitaji kuwa na mtaalamu anayeweza kusimamia manunuzi ili tuweze kupata faida ya manunuzi kutoka kwa wauzaji mbalimbali. Lakini hebu tutazame thamani ya vifaa vinavyowekwa katika nyumba za Serikali ambazo ni nyingi na zina thamani kubwa. Tunahitaji wataalamu ili waweze kununua kwa bei nzuri yenye thamani.

Tujikumbushe hata ununuzi wa rada uliotokea je, wataalamu walishirikishwa katika ununuzi wa vyombo kama hivi? Dhamira yangu ni kuonyesha kwamba tunatumia fedha nyingi sana katika manunuzi hivyo tunahitaji wataalamu washirikishwe katika manunuzi. Tunahitaji vilevile wataalamu kwa mfano katika huduma za usafiri kwa sababu utaalamu huu sio wa kununua vifaa tu, utaalamu unakwenda mpaka katika ununuzi wa huduma. Huduma za usafiri kwa mfano Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)* linakodisha ndege kwa ajili ya huduma za usafiri, anahitajika mtaalamu atakayesimamia ununuzi wa huduma kama hizi kwa sababu ukodishaji wa ndege ni gharama kubwa kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii mpya inapiga hatua moja mbele zaidi, maana yake inaongeza zaidi ya majukumu yaliyokuwepo katika sheria iliyopita na sasa inaongeza majukumu hayo. Hivi sasa sheria hii pia inaelekeza usimamizi katika kazi za makandarasi ambazo zinachukua fedha nyingi sana. Kwa hiyo, sasa sheria inaelekeza nguvu zake huko ili kusimamia wataalamu wanaohusika na huduma hizi za ukandarasi. Sasa kazi ya ukandarasi ni pamoja na ujenzi wa majengo lakini vilevile na ujenzi wa barabara. Barabara ziko katika ngazi mbalimbali za Serikali Kuu, ziko barabara za Mikoa na Wilaya. Kwa hiyo, umuhimu wa sheria hii sasa unazidi kuongezeka lakini shabaha ni kuwa na uhakika kwamba tunaweka nguvu zetu zote katika kusimamia na kupata thamani ya fedha tunazotoa kwa ajili ya mahitaji ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuonyesha umuhimu huo hebu tuangalie ni maeneo gani ambapo tunaona sheria hii au ile ya zamani imekuwa ikitumika vibaya. Tukitazama kwa mfano matumizi ya fedha za MMEM na MMES, unapoyatazama kuyachambua kutoka katika ngazi ya shule utaona kwamba ni shilingi 3,100,000 zinazotolewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa hizi zinaweza zikaonekana ni fedha ndogo. Lakini ukiutazama kwa mpango mzima kwa wilaya, mkoa, kitaifa ni fedha nyingi sana. Kwa hiyo, tunasema nini kuhusu matumizi ya fedha hizi ambazo ni kubwa kwa kiwango kikubwa Kitaifa lakini zinashuka chini kwa matumizi yanayoonekana viwango vyake ni vidogo na havibanwi ndani ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo katika fedha za Mpango wa MMES ni kitu gani ambacho kinatokea. Mimi nakiita potofu katika matumizi ya fedha za namna hiyo na jinsi ambavyo baadhi ya wale ambao sio wataalamu na wakati mwingine hata wataalamu wenyewe wanashiriki katika kufanya hayo mambo ambayo mimi nayaona potofu. Tunapotakiwa kununua bidhaa pengine sheria inatulazimu tutafute angalau *quotations* kutoka kwa zaidi ya muuzaji mmoja. Je, wataalamu na wale ambao sio wataalamu ambao ni wengi zaidi wanaofanya kazi hizo kwa kutumia fedha za Serikali

hivi kweli wanafanya kazi hizo kwa uaminifu? Hivi kweli wanakwenda katika maduka mbalimbali kiutaratibu na kwa uaminifu kutafuta q*uotations* hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ushahidi unaoonyesha kabisa kwamba zaidi ya asilimia 50 hawafuati taratibu hizo kwa kanuni na uaminifu, wanavyo vitabu vyao wenyewe vya *proforma invoice*. Kwa hiyo, wenyewe wanajiandikia *proforma invoice* zinazotakiwa tatu. Wote wanaandika na wanapeleka pale na wanaamua tu wanataka kwenda kununua wapi. Wanaweka kiwango cha bei wanachotaka na zile nyingine zinakuwa zaidi ilimradi manunuzi yafanywe katika mojawapo ya maeneo wanayoyahitaji. Nasema huu ni utendaji ambao unatuharibia kwa sababu unatuelekeza katika kutumia vibaya fedha za Serikali. Tunatumia fedha nyingi zaidi za Serikali kuliko thamani ya vitu tunavyovipata kwa matumizi halali ya Serikali, jambo hili la hatari kubwa sana.

Nasema linafanywa na baadhi ya wataalamu na si wote, lakini linafanywa zaidi na wale ambao sio wataalamu na ukienda katika mpango huo wa fedha za MMES huko ndiko utakakoshuhudia jinsi haya yanavyofanyika. Si kweli kwamba sisi kama viongozi hatufahamu, wengi wetu tunafahamu, tutachukua hatua gani kuzuia? Wataalamu wanaweza wakapatikana lakini hebu tuangalie katika Halmashauri zetu maeneo ambayo sasa fedha nyingi za Serikali ndiko zinakoelekezwa huko; je, huko nako wapo wataalamu watakaokuwa na uwezo wa kusimamia fedha hizo kitaalamu kufuatana na jinsi Muswada huu unavyotuelekeza?

Zipo Kamati zinazoitwa Kamati za Tenda, zile wakati mwingine thamani ya kazi wanazohitaji kufanya ni zaidi ya shilingi milioni 100. Je, tunao wataalamu kweli? Ndani ya Halmashauri zetu wanaopaswa kuweza kusimamia tenda hizo kisheria tunapozungumzia na kuelekeza nguvu zetu kwenye makandarasi, wapo? Tunafanya nini sasa kama Serikali Kuu kuzisaidia Halmashauri zetu ili zisije zikaingia mahali pabaya zikabanwa na sheria hizi au Halmashauri zikaendelea kutofuata taratibu na kanuni na msimamo wa sheria zetu sisi wenyewe na Halmashauri ni vyombo vikubwa vya Serikali? Kama tulivyozisaidia Halmashauri katika kutafuta wataalamu wa Mahesabu, Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani basi ningeomba vilevile Serikali iangalie sasa kuhakikisha fedha za Serikali zinatumika vizuri kuzisaidia Halmashauri zetu kupata wataalamu hao watakaokwenda kusaidia katika utekelezaji wa sheria hii muhimu ambayo kwa hakika sisi wote tunaiona kwamba ni muhimu sana. Vinginevyo tutakuwa na sheria lakini sheria hii haitatumika katika maeneo mengi kama tunavyokusudia. Nilikusudia kusema hayo machache, naomba niseme kwamba naunga mkono sana Muswada huu. Nina uhakika utatusaidia lakini tufanye dhamira ya kuhakikisha kuwa wataalamu wanapatikana na wanafanya kazi zilizokusudiwa kwa uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, narudia tena naunga mkono Muswada huu. Ahsante.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia Muswada huu muhimu. Mimi nina machache tu ya kuzungumza, lakini kabla ya hapo ningependa nijumuike na Wabunge wenzangu kutoa

rambirambi zangu kwa marehemu Waziri Salome Mbatia na natoa pole kwa ndugu zake wote na pia kwa Wabunge wenzetu ambao wamepata shida mbalimbali, waliofiwa na mama zao kama Mheshimiwa Mkullo na Mheshimiwa Hamad Rashid. Vilevile Mheshimiwa Yono Kevela, kwa kufiwa na watoto wake pamoja na matatizo mengine mengi ambayo Wabunge wanayo kama wanadamu.

Kwa nafasi hiyo pia ningependa kutoa rambirambi zangu kwa yule dereva ambaye alikuwa anamwendesha Mheshimwa marehemu Mbatia, maana naye pia ni mwanadamu ingawaje hatajwitajwi lakini Katiba yetu inazuia ubaguzi, kwa hiyo na mimi namtaja pamoja na ndugu zake wote nawapa pole kwa sababu alipata hayo katika juhudi za ujenzi wa Taifa pamoja na yule utingo aliyekuwa kwenye ile *Fusso,* wote Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu Watanzania wote wanauangalia kuona kwamba utabadilishaje hali ambayo ilikuwa imezoeleka kuendelea. Kwa sababu haya mambo ya *procurement*, ugavi, ununuzi wa vifaa, hili eneo ndilo limeleta tatizo kubwa katika uchumi wetu kwamba mali ya wananchi imepotelea katika taratibu kama hizo na sio siri kuanzia ngazi za Serikali Kuu hadi Serikali za Mitaa, pesa za wananchi zimekuwa hazina udhibiti kwa sababu taratibu zinazotumika katika Ununuzi na Ugavi wa Vifaa unakuwa kama shimo ambalo linapoteza fedha za walipa kodi wa nchi hii. Kwa hiyo, kwa kutumia kifungu cha Katiba ambayo tulikubaliana kwamba ndio itakayoendesha nchi hii kifungu cha 27(2) kinasema kwamba: "Watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na ya pamoja kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao." Kwa hiyo, Bodi hii kuteuliwa na kusimamiwa na Serikali peke yake ndilo upungufu mkubwa ambao nimeuona hapa. Kwanza kabisa isingefaa kiongozi wa Bodi hii ateuliwe na Rais.

Kwa sababu mara nyingi hizi Bodi au vyombo ambavyo vinasimamiwa na Ofisi ya Rais utendaji wake unakuwa ni wa kutii mamlaka ya mtu mmoja na kwa hiyo kufanya kazi kwa kadri anavyotaka yeye. Na hili nawaomba Wabunge waje waliangalie katika marekebisho ya Katiba kwa sababu tukiangalia kama *PCCB* inakosa meno kwa sababu inabidi amri ya kumkamata mtu lazima itoke kwa Rais. Kwa hiyo, hii nadhani inapunguza uwezo wa…....!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATLIDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu………! Kanuni ya 55, jambo analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge ni jambo ambalo sio sahihi, napenda afute kauli yake kwamba kuweza kumshika mtu *PCCB* inabidi ipate mamlaka na kibali kutoka kwa Rais, sio kweli! Naomba afute, na sio kweli kwamba Taasisi zilizoko chini ya Mheshimiwa Rais hazifanyi kazi vizuri kwa sababu zinafuata amri ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *Chief Whip* ametoa hoja akimwomba Mheshimiwa Chacha Wangwe afute usemi wake. Vilevile niongeze kwamba kanuni zetu pia hazituruhusu kujadili mwenendo wa Rais ndani ya Bunge na sheria mama pia

inakataza hivyo kujadili mwenendo wa Mheshimiwa Rais wetu ndani ya Bunge letu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Chacha Wangwe nakuomba usimame ufute kauli hiyo na uendelee kujikita kwenye Muswada na sio tena kujadili mamlaka na shughuli za Mheshimiwa Rais ndani ya Bunge.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa hayo maelekezo. Nilikuwa najaribu kuchambua kipengele kile cha Katiba lakini basi ninaiondoa kwa imani ya kwamba *message sent and delivered. (Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, naomba ufute kauli yako na hatuendelezi mjadala kwa uliyoyasema kwa kufuata unachokizungumza. Tunaomba ufuate utaratibu, unafuta kauli yako unaendelea na hoja yako.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nimefuta kauli yangu, naomba niendelee na hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Nakuruhusu sasa endelea!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Bodi hii kusimamiwa kwa kiasi kikubwa na Waziri, ningeliomba Bunge liangalie umuhimu wa kuhusisha vyombo vingine ambavyo pia ni vya wataalamu kama *Chamber of Commerce* au chombo kama cha *Institute of Engineers* au hata chombo kama vile kinachosimamia Makandarasi. Chombo cha Makandarasi ili waweze ku-*monitor* mienendo ya hii *council* ambayo inataka kuteuliwa kwa sababu wakiwa wenyewe kama watu wa Serikali na kwa sababu Serikali kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba Serikali haina uwezo wa kujidhibiti basi lazima kuna upungufu utakaojitokeza.

Naomba hilo liangaliwe ili kusudi utendaji uweze kuwa mzuri zaidi na vilevile kiwango kama hiki cha kusema kwamba Kampuni inaweza kuajiri huyo mtaalamu iwe na *turnover* ya kama milioni 200. Hiki ni kiwango kidogo na pengine hakitaweza kukidhi kuwaajiri wataalamu ambao wana uwezo mkubwa na kwa kuongezea hapo ningesema kwamba suala lisiwe tu kwamba ni kwa ajili ya wataalamu, ni lazima tuzingatie mtaalamu anahitaji kuwa na maadili na uadilifu wa kutosha kwa sababu kigezo cha utaalamu peke yake hakitoshi kumfanya kiongozi awe mwadilifu. Ndiyo maana hata katika maadili ya uongozi haijatajwa utaalamu, ila *integrity* ya mtu mwenyewe katika roho yake.

Kwa hiyo, hili nalo liangaliwe kwamba wale watakaohusika wawe waadilifu ili yasiendelee yale ambayo tumeona katika Halmashauri zetu. Kwa mfano, kama alivyosema Mheshimiwa mmoja aliyenitangulia hapa kuwa fedha za wafadhili kwa mfano zinazokuja kama za MMES katika mambo ya *Procurement* ndio zimepotea tena na MMEM. Hata vifaa vinavyonunuliwa kwa wale wafadhili wanaotoa misaada wanahakikisha kwamba wale ambao wanakuwa wanunuzi wa vifaa hivyo wanakuwa wa nchi zao. Hawa wataalamu wana jukumu pia la kuangalia kwamba wanunuzi wa ndani

nao wanafaidika kutokana na hii biashara na vitu vile vinavyonunuliwa viwe vya *standard* ya juu kulingana na *Bureau of Standards* inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba tuangalie utendaji wa nyuma wa hizi *Procurement.* Kwa mfano, imewahi kusemekana kwamba hata meli mbovu zimewahi kununuliwa kama mpya, rada mbovu zimewahi kununuliwa kama mpya na hayo yote ni kutokana na haya mambo ya *Procurement.*

Kwa hiyo, ningeshauri kwamba kuwe na *transparency and accountability* ya kutosha kwa sababu wananchi nao kulingana na hicho kipengele nilichosoma cha Katiba wanahitaji kujua kinachoendelea na sio baadaye wanaambiwa kwamba fedha zilipotea. Kiweze kuwa ni chombo *transparent* na hayo mambo yake yawe yanawekwa wazi kwa Bunge kufahamu na wananchi wote kwa ujumla kuhusu manunuzi ya vitu mbalimbali katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kueleza, hayo nadhani yametosha, natumaini kwamba yatafanyiwa kazi na Serikali. Ahsante sana. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hebu ninaomba niendelee kusisitiza. Nisisitize maamuzi yangu ya kumfanya Mheshimiwa Chacha Wangwe asitishe kauli yake na aiondoe katika mjadala wetu wa leo.

Naomba niwakumbushe kuwa Kanuni Namba 50(6) inasema, "Isipokuwa tu kama kunatolewa hoja mahususi kuhusu jambo hilo, itakuwa ni marufuku kwa Mbunge yeyote katika mjadala wowote Bungeni kuzungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Majaji, Mahakimu au watu wengine wanaoshughulika na utoaji wa haki. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba kuendelea kusisitiza kuwa tunapochangia hoja zetu humu ndani ni lazima tuwe makini sana. Namshukuru Mheshimiwa Chacha Wangwe kwa kuondoa hoja ya kujadili mwenendo wa Rais ndani ya Bunge letu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii kwa kifupi tu. Kwanza, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake ya Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wakuu wa Wizara hiyo kwa kuleta Muswada huu unaokusudiwa kutunga sheria ya wataalamu wa ununuzi na ugavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Muswada huu ulitakiwa ungekuja hata juzi kwa ajili ya umuhimu wa eneo hili la ununuzi na ugavi. Kwa muda mrefu sana tumekuwa tukitilia mkazo na msukumo kwenye eneo la Uhasibu na Uhandisi lakini hawa wanafanya kazi karibu na wanunuzi na wagavi. Kwa hiyo, nadhani msisitizo sasa hivi tungeweka zaidi kama ulivyoletwa na Serikali kwenye eneo hili la ununuzi na ugavi, huku ndiko ambako kuna mambo mengi sana yanaweza kufanyika na yakawatia kwenye matatizo wahasibu pamoja na wahandisi.

Katika ununuzi kwa kweli ndiko ambako kuna vituko vya manunuzi hewa, kuna upungufu wa kutofuatilia vitu ambavyo vimeachwa wakati wa manunuzi. Kwa sababu mtu anaweza kutoa *order* lakini anapokwenda kuchukua vifaa, akaambiwa vifaa kiasi fulani havipo. Sasa kuna upungufu katika kufuatilia. Kwa eneno hili kwa kweli taaluma hii ingetiliwa mkazo na tutafanya jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mntangi nisingependa azungumze aliyosema lakini ametoa maelezo kwamba karibu asilimia 90 ni ununuzi ambao unapitia kwenye wanunuzi hao pamoja na wagavi. Lakini mimi kuna moja ambalo nilitaka tulizungumze hapa. Kwa sababu kununua na kugawa si mwisho wa tukio hilo. Hivi vifaa vinavyonunuliwa na kwenda baada ya hapo vinakuwaje? Mimi nadhani katika Sheria hii ya Ununuzi ingekuwa ni ununuzi, ugavi na utunzaji. Kwa sababu tunanunua vitu vingi tu, tena kwa fedha nyingi lakini baada ya hapo pengine hatuendelei zaidi. Baada ya kuingiza kwenye vitabu basi tumefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pengine tuanzie hapa hapa kwenye Bunge. Hivi hapa tumeshaandaa *schedule* ya matengenezo? Maana wameshamaliza hawa je, viti hivi tunavyokalia vitachukua muda gani ili tujiandae tusingoje mpaka vipasuke? Kwa hiyo, nadhani hawa wataalamu mafunzo yao yaelekee huko kwamba ununuzi sio mwisho. Ni kile kitu ulichonunua kinatakiwa kikae kwa muda gani. Sasa ni nani ambaye anatakiwa afanye kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu kwa ujumla hatuna utamaduni wa matengenezo. Tukisema matengenezo pengine inapotoshwa hiyo. Kuna neno mara nyingi linatumika hili la ukarafati. Kuna tofuati ya ukarafati na ukarabati. Ukarafati ni kwamba kitu kipo kinatakiwa kikarafitiwe yaani ukitunze kama ulivyo mwili wa binadamu. Nywele ukiziacha itakuwa matatizo, baadaye watu watakushangaa wanaanza kukupa majina mengi tu, kwamba huyu labda kichaa au nini. Sasa kama mwili tunaufanyia ukarafati wa namna hiyo maana si ukarabati maana ukarabati kimeharibika, *repair* unakwenda kutengeneza. Sasa nadhani fani hii isisitizwe na pengine hata katika Sheria. Majukumu anayopewa ni ununuzi, ugavi na ukarafati kwa maana ya *maintenance* si ukarabati wakati kitu kimeharibika.

Ukichukua mfano wa gari, mnunuzi ametoa *order*, limenunuliwa limekabidhiwa kwa mtumiaji. Baada ya hapo kunafuata nini? Linatakiwa lipelekwe *service* kwa kiwango fulani, likitimiza maili fulani, kitu fulani lazima kiondoke. Sasa hawa nadhani tusiishie kwenye ununuzi na kugawa, wafuatilie vilevile matengenzo na utunzaji wake. Ninadhani pengine katika Sheria tungeangalia Mheshimiwa Waziri kama kuna mahali pa kuliweka hili. Tujenge utamaduni wa ukarafati. Kwa Kiingereza ningesema, *there is absence of culture of maintenance*. Ukishanunua kitu unakiacha kijitunze chenyewe ambacho bado kitakuwa na gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya ambayo yanaungana vizuri sana na matumizi makubwa ambayo yanakwenda kwenye maeneo hayo ya ununuzi na ugavi, sasa napenda kwenda kwenye Muswada wenyewe. Nina mchango katika kifungu.

Sasa hapa mimi sijui tunatumia Ibara katika kifungu. Mimi nitatumia kifungu, ukiwa na kifungu maana kuna ile Sehemu halafu kifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye Kifungu cha 12 cha Sehemu ya Tatu ukurasa wa 11, kile kinachomhitaji yule Msajili *(Registrar)*, kifungu kidogo cha (2). Tukubaliane na Mheshimiwa Waziri kwamba tungetoa muda *specific* kwa sababu katika eneo hili linalosema: *"The Registrar shall enter the names of procurement and supplies professional entitled to have his names entered in the Register and such names shall be entered as soon as is practicable".* Sasa *"as soon as is practicable"* inaweza kuwa miaka miwili ndiyo *practicability"* yenyewe hiyo. Mimi nadhani ningempeleka Waziri kwenye kifungu chake cha 15 ambacho umekifurahia ambacho kimempa msajili kuwasilisha *application* kwenye Bodi yake katika muda wa siku 30. Mimi nadhani na huyu naye tumpe siku za kuandikisha na kuingiza katika vitabu. Mimi ninapendekeza siku 14 na tuondoe ile *as soon as is practicable.* Inaacha nafasi kwa mtu kujitetea kwamba mimi nilivyoona ndivyo hivyo. *As soon as is practicable* inaweza kuwa miaka miwili au hata unaiacha tu maana yake bado haijaingia vizuri kwamba hiyo inaweza kutekelezwa katika kifungu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulichangia hapa ni Kifungu cha 46, ukurasa wa 26, hiki kinasema: *"no person shall employ or continue to employ, in procurement or supplies activities, a person who is not a registered as a Procurement and Supplies Professional*". Sasa hapa nadhani katika kifungu hiki tuangalie mahali pa kuweka muda kwamba kama yupo mtu anafanya kazi hiyo hana utaalamu basi mtu huyo apewe muda au aliyemwajiri apewe muda wa kuhakikisha kwamba mtu huyo anafikia kiwango kile kinachohusika; na hapa tungeunganisha na muda unaotakiwa.

Kwa mfano, kama ni *Supplies Assistant* anatakiwa awe amechukua mafunzo yanayochukua muda kama mwaka mmoja basi apewe muda huo kwamba katika mwaka mmoja huyu mtu awe amejifunza amefikia hiyo *qualification* inayohusika. Kwa sababu tumepata takwimu kwamba watu hawa ni haba, kwa hiyo, ukiwaondoa tu kwa kutumia Sheria kwamba hana hiyo bila kuweka kipengele kingine kwamba yule aliyepo ambaye anafundishaka basi katika muda ule wa kuchukua kozi kama ni mwaka mmoja basi apewe masharti hayo katika mwaka mmoja huo awe amemfundisha huyo ili aweze kuendelea vinginevyo baada ya muda huo kupita itakuwa tatizo.

Halafu katika kifungu cha 47, ambacho kina *amendment*, lakini mimi siendi kwenye ile *amendment* nakwenda kwenye kifungu kidogo cha (4) kinachoeleza kwamba: *"a person referred to under sub-section (1), shall cause to be kept stock records which shall be maintained by Procurement Specialist and Supplies Professional."* Sasa hapa ndipo ninapotaka kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba tungeingiza ile *culture of maintenance*.

Kwamba hapa hapa katika kuweka rekodi afuatilie vilevile na utunzaji wa hivyo vitu. Asiishie hapo tu kuingiza kitu cha kuhakikisha kwamba *there is proper maintenance* au ukarafati kwa lugha yetu ya Kiswahili. Tukifanya hivyo tutaisaidia sana Serikali

katika maeneo mengi sana ambayo pengine hayana mtu. Ukishajenga au ukishanunua ukishakabidhi unaondoka lakini gharama iko pale pale, watakuja kuuliza tulinunua kitu kwa gharama hii lakini mbona hakijadumu mpaka sasa kumbe tatizo ni kutokuwa na ile *culture of maintenance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja hii ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKETI:** Mheshimiwa Shellukindo, nakushukuru sana kwa kuchangia hoja hii. Waheshimiwa Wabunge sasa namwita Mtoa hoja ili aweze kuzungumzia ushauri mbalimbali uliotolewa na Wabunge kwenye hoja yake.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja hii. Nianze kwanza kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii. Nianze na Msemaji wa Kamati ya Miundombinu, Mhesimiwa Rosemary Kirigini, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Chacha Wangwe na mwisho kwa kutajwa lakini si kwa umuhimu ni Mheshimiwa William Shellukindo.

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba tumeridhishwa sana sisi Wizarani. Kwanza, salamu za pongezi ambazo zimeletwa kwetu. Lakini sisi kama viongozi wa Wizara tunazichukua kwa niaba ya watendaji wote wa Wizara pamoja na Taasisi zake tunawashukuruni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni ushauri mwingi umetoka kwenye michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, lakini lipo moja tu ambalo lilitoka kwenye Kambi ya Upinzani, yawezekana tuna mtazamo tofauti kwa uelewa wa suala hili. *Independence* kutokana na nini? Chombo hiki kwa kuwa chini ya Serikali kitakuwa huru kiasi gani?

Chombo hiki kama tulivyoeleza tunasema tofauti na chombo kilichopo hivi sasa, tunataka tukiimarishe kwa kuweza kuisimamia vizuri hii kada ya wataalamu hawa wa manunuzi na ugavi. Tumepanua isiishie kwenye vyombo vya Serikali, sasa tusichanganye uhaba wa wataalamu hawa na umuhimu wa kuwa nao katika vyombo hivi kama kweli chombo hicho kiwe ni taasisi ya Serikali au binafsi, maana ni lazima upate. Sasa kama unataka ulione katika mapana hayo nadhani utaelewa hoja hiyo haihitaji hii dhana ya *independent from* Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Kamati ya Miundombinu kwa hayo waliyoyasema, nadhani tulisikia hoja hiyo ya kwanza thamanisho la *assets*. Ndiyo tumeiweka wazi halafu tukaenda kwenye *turnover*. Ukisema *turnover* ya shilingi milioni 150 ni ndogo kwa hali ya Tanzania nadhani kidogo labda sijui tunaishi katika dunia ipi?

Lakini hili lilizungumzwa kwa ufasaha sana kwenye Kamati na ndiyo maana nashawishika kuliomba Bunge lako Tukufu likubali hayo marekebisho ambayo tumeyaleta yabaki kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wasiwasi wa Waziri kwamba anaweza akatoa adhabu tofauti na zile ambazo zimetajwa na Sheria ya Msingi. Haiwezekani hata siku moja itakuwa ni *auto-violence,* itakuwa ni kinyume kabisa na Sheria, kisomeni vizuri kifungu hicho cha 29 kinakupeleka kwenye 24, halafu ndiyo uje kwenye 29. Kwenye 24 inakwambia, *if any Procurement and Supplies Professional* anapatikana na hatia kwa makosa yaliyotajwa bayana katika Sheria hii.

Ukisoma utaona yamekwishaainishwa, hayo ndiyo yanayosemewa na baada ya uchunguzi utakaofanywa na Bodi akapatikana kuwa na hatia ya kufanya tendo au kutotenda ndiyo yanaainishwa hapo. Matokeo yake Bodi itafanya nini? Inaweza ikampatia onyo, inaweza ikaagiza jina lake liondolewe katika *Register*.

Sasa ile ambayo inawasumbua Waheshimiwa Wabunge 29, ni ile ameitwa amepelekewa *summons* kwa yale ambayo anatuhumiwa nayo kwa mujibu wa kifungu cha 24 na anakaidi au anasema huyu naye ni nani kuniita mimi. Wapo wa namna hiyo tunawajua, basi nasema sasa ukaidi huo, huo *ujogoo jogoo,* hasa na wenyewe ushughulikiwe. Utashughulikiwa vipi, ni kwa mujibu wa Kanuni ambazo mamlaka husika itaweka.

Lakini kuna kinga ambayo inatolewa kwenye kifungu kidogo cha 29(ii) kwamba ushahidi ambao atatakiwa huyo muhusika autoe mbele ya Bodi au hati atakayotakiwa aitoe mbele ya haki basi apewe kinga ile ile ambayo angeliipata iwapo ushahidi huo au hati hiyo angeliitoa mahakamani, ndiyo kifungu kidogo. Kwa hiyo, unaona inalinda pande zote mbili, hivyo sioni wasiwasi ambao umeelezwa na Waheshimiwa Wabunge kwenye eneo hili. Ukiisoma kwa mtiririko huo wala hakuna tatizo hata kidogo.

Sifa za Msajili ziwekwe wazi. Huyu mamlaka husika inayoteua hiki ni kifungu cha 9. Kwanza tumekifanyia marekebisho ili kukifanya kiwe wazi zaidi. Lakini nasema *Public Officer* haitoi sura ya kuwa na sifa hizi kwa maana kwamba wanataka huyu Msajili wa chombo hiki ambaye pia atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu na yeye awe na sifa hizi. Sawa kabisa. Nitashangaa kidogo. Labda hoja hapa ni kwamba tuione basi imeandikwa hivyo katika Muswada. Lakini unataka umwone mtu wa namna hii afanane na ile Kada ambayo anaisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kama ninavyoifahamu, hata mifano iliyotolewa Bodi ya Makandarasi, Bodi ya Mainjinia iko chini ya Wizara hii, zina sheria zake. Kwa hiyo, tunajua kile ambacho kinapaswa kifanyike unapotumia maneno haya *Public Officer* lazima akidhi pia sifa za chombo ambacho anakwenda kusimamia.

Namshukuru sana Mheshimiwa Herbert Mntangi, ameyasema yale ambayo mimi ningeliyasema kwa sababu tumekuwa tunayasema kila mwaka hapa, fedha nyingi za umma zinakwenda kwenye manunuzi haya, ugavi huu, sasa usipoweza kuzisimamia

vizuri tatizo linaanzia pale. Namwelewa sana, tena tunamshukuru sana kwa sababu hii Kada kweli jamani hatujaweza kujenga uwezo mpana.

Wapo wachache akina Profesa Dr. Mahanga wamo Bungeni humu, wako na wengine. Lakini ni wachache, tunafanyaje katika kuzisaidia Halmashauri zetu ili ziweze kufanya maamuzi yanayolengwa na kuona na manufaa ambayo yanalengwa na Muswada huu. Hii ni changamoto ambayo tunayo Serikalini kwa maana kwamba lazima tuendelee kuwafundisha hawa wataalamu wa namna hii, tuwe nao kwa wingi, tuwapatie marupurupu mazuri, wasiweze kuvutiwa kwenda mahali pengine. Lakini lengo ni hilo hilo kama tulivyofanya kwa Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani. Lengo la Serikali ni kuimarisha chombo hiki.

Kwa nini chombo hiki kipate fedha za Serikali? Madaktari chombo cha Wanasheria hawapati. Hii hoja pia imesemwa na wenzetu. Kwanza Sheria ya sasa ya 81 ilikuwa na dhana hiyo hiyo kwa sababu unataka ukilee chombo hiki. Tunaendeleza dhana hiyo hiyo kwa sasa na vyanzo vimetajwa ni vilevile ukiangalia kifungu cha Sheria ya sasa utakuta *concept* ni hiyo hiyo.

Ukishakubali kwamba ni wachache, halafu hapo hapo unasema wao wenyewe wasije wakajisaidie watafute fedha zao, sasa unataka uwaumize kabla hata hawajaanza. Lakini mpaka sasa hivi huwa tunakuja Bungeni humu kuomba ruzuku, ndiyo imekuwa inatokea hivyo kwa utaratibu wa sasa na tunataka tuendelee na utaratibu huo.

Mheshimiwa Shellukindo, matengenezo, *culture* ya *maintenance* ambayo inaonekana huwa tunaisahau sana, mimi nakubaliana sana. Siko mbali sana kwa hilo. Lakini hawa labda tu niseme ukisoma kifungu cha 48 cha Muswada unapata ule mtiririko ambao unakufikisha katika hayo hayo ambayo unataka uone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa ni ku-*track down,* vile vitu umevinunua, umevisambaza, lakini kabla ya kuvisambaza umevitunza vipi na kule vilikopelekwa vinatunzwa vipi. Sasa kifungu cha 48 ndicho kinaweka utaratibu wa *stock authorization* ya *certification* ambazo zinatakiwa kwa masuala mazima ya matunzo ambayo kwa maneno tofauti ameyasemea Mheshimiwa Shellukindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingelipenda nichukue muda mwingi kwa sababu hoja hii imeeleweka, tumeungwa mkono. Nimalizie tu kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa haya mliyoyasema. Ushauri mzuri tumeuchukua, haya mahususi ambayo ni ya kiuandishi huwa namwachia Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wake. Lakini tumefurahishwa sana na michango yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Pili*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hatua inayofuata sasa ya kupitisha kifungu kwa kifungu. Namwomba sasa Katibu atuongoze.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi wa Mwaka 2007 (*The Procurement and Supplies Professional Board Bill, 2007)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3
Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 12(2), nilikuwa nimetoa ushauri. Nataka tuafikiane na Mheshimiwa Waziri kwamba katika kifungu cha 15, ile Bodi imepewa siku 30 za kushughulikia. Sasa hapa nina mapendekezo kwamba basi na huyu katika kuingiza asiachiwe wazi tu; *"as soon as practicable"*, tungeweka siku 14. Hilo ndilo wazo langu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ushauri wa kutoa tena muda muafaka kama ulivyotolewa katika kifungu kile cha 15!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa ushauri wake. Lakini yale maneno *"as practicable after being accepted by the Board for registration"* ndiyo yanayotoa ule unyumbulifu. Inaweza ikawa ni siku moja, siku mbili, kwa kutegemeana na makando kando ya suala lenyewe. Ndiyo maana maneno hayo yana maana yake sana katika sheria. Tunaomba tu yabaki kama ilivyo, lakini uharaka ni ule ule wa kuweza kutekeleza maamuzi.

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 28
Ibara ya 29

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba ufafanuzi zaidi kuhusu kifungu cha 29 kwamba adhabu itatolewa kwenye kanuni zitakazotungwa na Waziri, siyo sheria kama inavyosema. Sasa naomba ufafanuzi; iwapo Waziri amechelewa kutunga hizo kanuni na makosa yametendeka ni adhabu gani itatolewa, kwa kuwa kanuni zitakuwa hazijatungwa? Kwa hiyo, naomba ufafanuzi zaidi kwa kifungu cha 29.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kanuni zitakuwa hazijatungwa kwa kosa hilo, basi hakuna adhabu itakayotolewa kwa kosa hilo kwa sababu hazijatungwa. Shabaha hapa ni mamlaka hiyo itunge kanuni ili kutekeleza sheria. Hoja za Wabunge waliochangia ilikuwa ni kwamba kifungu hiki kinampatia Waziri mamlaka ya kutoa adhabu kwa makosa hayo ambayo yameainishwa, basi adhabu hiyo tuione hapa. Nimejaribu kufafanua kwamba anza kusoma kwenye kifungu cha 24. Ukianza kwa mtiririko huo, wala hakuna tatizo. Lakini ukianzia hapa, unapata tatizo.

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimetoa ushauri kwamba watu hawa ni wachache na kuna ambao wanafanya kazi hizo bila kuwa na taaluma inayotakiwa. Sasa nataka tu kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, labda kama ataweka hilo wazo nililotoakwenye kanuni, basi sina tatizo. Lakini tukiliacha tu hivi hivi, tuchukue kwa mfano, Halmashauri yangu ya Wilaya ya Lushoto, pengine kuna mtu anashughulikia masuala ya ununuzi na ugavi, lakini hana taaluma inayotakiwa, sasa hapa kifungu cha 46 kinasema: *"no person shall employ or continue to employ...."* Ukiacha wale *trainees* ambao wameelezwa chini huku nasema pengine pangekuwa na muda hapa na muda huo anaopewa, kama utakuwa kwenye kanuni, sawa, lakini pawe na mahali pa kumpa jukumu la kum-*train*, isije ikangojewa Serikali tu, kwamba "unamhitaji huyu, kwa hiyo, tunakupa muda wa miaka miwili," maana yake ndiyo wa kum-*train* mtu wa ngazi hiyo ili ichukuliwe hii katika lile jukumu hasa na uwajibikaji mzuri. Ni hilo tu nilitaka uhakika huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, suala la msingi ni *transition period* ya utekelezaji wa jambo lenyewe, tunafanya nini na uhaba wa wataalamu hao tulionao?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni hoja ya msingi sana. Hata kwa wataalamu kama *Accountants*, ukichukua sheria ya *NBAA*, kuna *authorized* na *approved Auditors* na *Accountants*. Lengo likiwa ni hilo hilo. Nadhani dhana hii tuione. Hoja ya Mheshimiwa Shellukindo ilikuwa inaanza kujibiwa kwenye kifungu kidogo cha 4, lakini pale ni kwa mafunzo. Katika hali ambapo unasema sisi hatuna hata mtu wa namna hiyo katika Halmashauri yetu, tufanyeje, tukodoleane macho tu? Nadhani ndiyo hoja kwamba *transition period* ingelikuwa wazi kabisa ili tusiweze kujiumiza sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna tatizo moja hapa. Tupo kwenye Kamati ya Bunge Zima, hatujaletewa mapendekezo ya marekebisho mahususi na mimi sina lugha ambayo naweza nikaiweka ambayo itaingia kwenye *Hansard*. Lakini tuangalie sasa uwezekano wa kulifafanua hili kwenye kanuni. Tukija kwenye ukurasa wa 28 wa Muswada, naridhika kabisa kuna mahali kwenye kanuni ambapo Waziri anaweza akayafanya hayo. Kwa hiyo, tuko ndani ya utaratibu. Nakushukuru sana !

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakushukuru! Nadhani huo ndiyo ushauri mwafaka wa kulishughulikia wakati wa kutunga kanuni za kusimamia sheria mama.

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 47

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante! Ninaomba tu ufafanuzi kidogo kwenye hiki kifungu cha 47 kuhusiana na *assets and turnover* ya *worth 100 million*. Mimi ninaona hii *100 million* kwa biashara ya kawaida na kuajiri mtu wa *procurement and supplies* itakuwa ni vigumu sana. Labda Mheshimiwa Waziri atupe maelekezo au afikirie kuongeza kiwango hiki. Asante!

**MWENYEKITI:** Asante. Kifungu hicho kina marekebisho. Nadhani kimekwishakuwa *considered*. Mheshimiwa Waziri, labda hapa una neno la kusema?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Serikali ilichukua ushauri wa kwenye Kamati na ndiyo maana tukaja na *schedule of amendments* kama inavyoonekana. Tuseme kwa upande wa rasilimali zenye thamani ya shilingi milioni 200 au *turnover* yenye thamani ya shilingi milioni 100, atakiwe sasa ku-*employ* angalau *procurement* na *supplies professional* mmoja katika shughuli zake za msingi *(procurement or supplies activities)*. Inawezekana sijamwelewa sana Mheshimiwa Kirigini, lakini sisi tulidhani kwamba kwa kufanya hivi tumekusanya kwa kuangalia hali halisi ya wafanyabiashara wa nchi yetu kwamba tutakuwa tumewahifadhi vizuri zaidi kwa viwango. Nakushukuru sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi wa Mwaka 2007 *(The Procurement and Supplies Professionals Board Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi wa Mwaka 2007 *(The Procurement and Supplies Professionals Board Bill, 2007)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi wa Mwaka 2007 *(The Procurement and Supplies Professionals Board Bill, 2007)*, sasa ukubaliwe. Naomba kutoa hoja!

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana. Tumeweza kupitia hatua zote za kupitisha Muswada huu ili uweze kuwa Sheria na uanze kutumika katika nchi yetu. Kwa hiyo, Muswada huu sasa unasubiri tu kibali cha Mheshimiwa Rais na utaanza kutumika kulingana na taratibu zinazotakiwa.

Niwapongeze, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako kwa kuweza kuhitimisha hoja hii sawasawa na salama na tuwatakie kila la heri katika utekelezaji wa Sheria hiyo mpya ambayo tumeipitisha leo katika Bunge letu. Vilevile niwatakie kila la heri katika shughuli nyingine nyeti inayokuja kesho. Mwenyezi Mungu awe pamoja nanyi wawili na wengine wote wanaoingia katika harakati hizo kesho za kinyang'anyiro cha uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli ambazo zilikuwa hapa mezani kwangu kwa siku hii ya leo, nafikiri tumezihitimisha zote. Lakini ninalo tangazo dogo tu hapa; naomba niwatambulishe kwenu, Viongozi wanawake wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), wajumbe 48 wakifuatana na viongozi wao wafuatao: Mohamed Utari - Mtunza Hazina, Feliciana Tarimo – Mjumbe wa Kamati ya Utendaji, Ruth Kiguhe – Mwezeshaji, Leornard Haule – Mwezeshaji na Dr. Leticiah Sayi – Mwezeshaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, viongozi hao wa Chama cha Walimu wako hapa Dodoma kuhudhuria Semina kuhusu UKIMWI. Kwa hiyo, waliona kuwa itakuwa vizuri angalau watembelee Bungeni na kuona shughuli zetu za Bunge zinavyoendeshwa na zinavyotekelezwa. Tunawakaribisha sana! Na isiwe tu kwa sababu ya semina, siku nyingine mkipata nafasi, walimu wetu, basi itakuwa bora mkitutembelea ili kutusaidia kuwaelewesha watoto wetu shughuli zinavyofanyika ndani ya Ukumbi wa Bunge. Karibuni sana Dodoma na karibuni sana Bungeni!

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, basi niseme shughuli zetu zilizopangwa kwa siku ya leo zote kwa kweli zimekamilika. Na hivyo basi, sisitishi Bunge, lakini nitaliahirisha mpaka Siku ya Jumatatu, saa 3.00 asubuhi ndani ya Ukumbi wetu huu wa Bunge. Asanteni na ninawatakia *weekend* njema! *(Makofi)*

*(Saa 6.52 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 5 Novemba, 2007 Saa 3.00 Asubuhi)*